SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Ajinyonga** akidhani ameua mume aliye mcharanga mapanga

UKURASA 4



**ALLEGRI: SIFAHAMU KAMA DYABALA ATABAKI JUVE**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Machi 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580892

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Samia afungua milango tume huru ya uchaguzi

• **Aagiza** kikosi kazi maoni kubainisha muundo wake utakavyokuwa... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kwa Mwenyekiti wa kikosi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

### TANZANIA, EU SASA KUREKEBISHA EPA

SERIKALI ya Tanzania imekutana na Umoja wa Ulaya (EU) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) ikiwamo...

UKURASA WA 4

### JAFO AFUNGUKA RIPOTI MTO MARA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amewataka wananchi kuepuka taharuki inayoendelea mitandaoni...

UKURASA WA 19

### MCHECHU AREJEA RASMI, AAHIDI MAKUBWA NHC

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, ameahidi kuondoa vikwazo mbalimbali vitakavyojitokeza ikiwamo...


## Kasi ajali bodaboda yamtisha Ummy

UKURASA 3

## Serikali yafuatilia uwapo kirusi kipya cha UVIKO-19

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA YAITANGAZIA 'KIAMA' GENDARMERIE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Samia afungua milango mapendekezo tume huru

**Na Jenifer Julius**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekiagiza kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vya siasa kuandaa mapendekezo kuhusu muundo wa tume huru ya uchaguzi.

Alitoa agizo hilo Ikulu, jijini Dar es Salaam jana wakati akipokea taarifa ya kikosi kazi hicho chenye wajumbe 25 kilichoongozwa na Mwenyekiti wake, Rwekaza Mukandara.

"Kuhusu tume huru mtatuletea mapendekezo, tume huru maana yake nini? Iweje? Lakini angalieni mifano ya waliokuwa na tume huru je, hawana migogoro ya kisiasa? Kwa mfano majirani zetu wanazo 'the so called' tume huru, je, wanaziendeshaje? Alihoji Rais Samia na kuongeza:

"Lakini tunaposema tume huru tunafuata nini hasa? Ni kitu gani kinatupa kiu tunahisi tutakipata kwenye tume huru."

**UHUSIANO VYAMA VYA SIASA VYOMBO VYA HABARI**

Rais Samia aliagiza kuboreshwa kwa uhusiano baina ya vyama vya siasa na vyombo vya habari ili kuwa na uhusiano wa karibu muda wote badala ya kuwaandika ifikapo kipindi cha uchaguzi pekee.

"Lakini mimi nilichokiona tukimaliza uchaguzi, miaka minne yote vyombo vya habari na vyama vya siasa wala hawana uhusiano sana, ule mwaka wa mwisho wanakusanywa wote UNESCO, pale vyombo vya habari mnafanya hivi na nyinyi vyama vya siasa mnasimama hivi hivi...hapo ndipo uhusiano una nawiri," alisema rais na kuongeza:

"Lakini huku miaka minne yote hakusemwi kitu, kazi kubwa inayosemwa ni kuisema serikali tu, sasa hivi nashukuru Mungu kazi nzuri ikifanywa mnasema mama kaupiga mwingi," alisema.

Kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kimependekeza Tanzania ianze harakati za kupata katiba mpya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Rais pia aliziagiza taasisi binafsi, vyombo vya dini na vyombo vya habari kutoa elimu kuhusu sheria na kanuni za vyama vya siasa na uraia ili wananchi waifahamu vizuri.

Kwa upande wa rushwa katika uchaguzi, Rais alisema inahitajika elimu kwa jamii, pia kufanyike uchunguzi kutambua chanzo cha tatizo hilo na namna gani wanaweza kuizuia, kuwa wote watoaji na wapokeaji wanashawishika kufanya hivyo.

"Natakwa niwaambie wajumbe, leo hii nikiwaambia mkasimamie majimbo mtazitoa kwa njia moja au nyingine, kwa sababu kuna nyinyi kuzitoa na wajumbe kuzitaka, kwa hiyo hapo kuna kazi kubwa ya kufanya, tufunge mioyo ya wajumbe, tufunge mioyo ya watoaji," alisema.

**AIGEUKIA TAKUKURU**

Rais Samia pia aliigeukia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa haifanyi kazi yake vizuri kwenye kudhibiti rushwa na kukiagiza kikosi kazi hicho kufanya uchunguzi na kuibua upungufu uliomo ili kuboresha utendaji kazi wao.

"Hili mlilolisema sio uongo ni la kweli, lakini tuambieni, ingawa mkisema wenyewe wanakasirika huko, ukisema Jeshi la Polisi halifanyi kazi vizuri unakwenda kujibiwa huko, hatufanyi kazi vizuri, huamini vyombo vyako, sasa nendeni, katizameni, katafuteni mtuambie," aliagiza.

Pamoja na mambo yalioainishwa, kikosi hicho pia kimependekeza harakati za kupata katiba mpya zianze baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Akisoma mapendekezo hayo, Profesa Mukandala alisema muda huo ni mwafaka kwa kuwa hautaathiri uchaguzi mkuu ujao.

Kadhalika kikosi hicho kimependekeza kufanyiwa maboresho kwenye sheria na kanuni za uchaguzi ili kuondoa migogoro inayojitokeza wakati wa chaguzi mbalimbali. Pendekezo lingine ni kuangaliwa upya kwa vigezo vya utoaji ruzuku kwa vyama vya siasa ambavyo vina usajili wa kudumu.



Balozi mpya wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza (katikati), akiwa pamoja na Naibu Katibu wa Biashara nchini Marekani, Don Graves (kushoto) na balozi mstaafu wa Marekani nchini Tanzania, Charles Stith, katika hafla ya kumkaribisha Balozi Kanza nchini humo, iliyofanyika kwenye ofisi za mwanasheria za Capitol Hill, Nelson Mullins, Washington DC na kuandaliwa na kampuni ya Pula Group. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania, EU sasa kurekebisha EPA

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI ya Tanzania imekutana na Umoja wa Ulaya (EU) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) ikiwamo baadhi ya vipengele vilivyoko ndani ya mkataba huo ambavyo serikali haikuviridhia.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao kilichohusisha wataalamu kutoka Tanzania na EU, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, alisema kutokana na serikali kutokukubaliana na baadhi ya vipengele hivyo katika mkataba wa EPA imeona ni vyema kukutana ili kuvifanyia marekebisho.

"Tumekaa na wataalamu wetu na wenyewe wamekuja na wataalamu wao, tutapitia kipengele kimoja baada ya kingine na tunaamini tutafika mwisho na kama tulivyo waambia wenzetu wa EU tunaona faida ya kufanya biashara na wao kwa maslahi ya pande zote mbili," alisema Prof. Kahyarara.

Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, alisema majadiliano hayo yanalenga kuangalia vipengele vya mkataba ambavyo Tanzania ilionyesha mashaka katika kikao kilichopita.

Alisema wanahitaji kuvipatia ufumbuzi vipengele hivyo na kusonga mbele kwa pamoja kutokana na kuwa Tanzania kwa sasa imetoa kipaumbele katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

"Itakumbukwa kuwa Tanzania inatekeleza Diplomasia ya Uchumi na wawekezaji kutoka EU wana nia ya kuja kuwekeza Tanzania na Afrika Mashariki, hivyo tukikamilisha majadiliano haya itakuwa ni jambo lenye maslahi kwa pande zote," alisema Fanti.

"Kikao cha leo (jana)' kinatokana na mazungumzo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan aliyafanya Februari mwaka huu alipokuwa katika ziara ya kikazi nchini Ubelgiji ambapo alikutana na Rais wa Baraza Kuu la EU, Charles Michael," alisema Fanti.

**Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, alisema majadiliano hayo yanalenga kuangalia vipengele vya mkataba ambavyo Tanzania ilionyesha mashaka katika kikao kilichopita.**

# Serikali yafuatilia uwapo kirusi kipya UVIKO-19

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inafuatilia uwapo wa aina mpya ya kirusi cha UVIKO-19 kilichothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema kirusi hicho, kinajumuisha kirusi cha Delta na Omicron, ambacho kimejiunda na kuwa kirusi kipya cha Omicron BA.1.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kufungua mafunzo ya wataalamu wa upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na ugonjwa mahututi yanayofanyika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Magonjwa ya Fahamu Muhimbili (MOI).

Alisema WHO inafanya utafiti wa kufahamu ukali wa kirusi hicho kipya na kwa upande wa wizara yake inaendelea ufanya utafiti kuwapo kwa kirusi hicho nchini.

"Nimeshawaelekeza wataalamu wetu waangalie tuone kama kimeshaingia nchini kwetu kwa sababu nchi nyingine wameshathibitisha," alisema Ummy.

Aliwasihi Watanzania kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na kirusi hicho. Alisema watu wengi wakipata chanjo watasaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo utakapothibitika kuwapo nchini.

Alisema hali ya uchanjaji bado ipo chini nchini kwa sababu asilimia 66 ya wanaougua UVIKO-19 waliolazwa hospitalini hawajapata chanjo, hali ambayo ni hatari kwa nchi na kusisitiza umuhimu wa Watanzania kujikinga na ujio wa kirusi hicho.

Alisema kama nchi nyingine ambazo kimeshatangazwa kuwapo, kuna uwezekano wa kuingia nchini kutokana na mwingiliano wa kibiashara katika mataifa mbalimbali duniani.

## HABARI KITAIFA

# Ajali za bobaboda zamtisha Ummy

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Mifupa na Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), inapokea majeruhi wa ajali za pikipiki 10 hadi 15 kila siku sawa na majeruhi 300 hadi 400 kila mwezi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya wataalamu wa upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na wagonjwa mahututi 270 yanayofanyika MOI.

Alisema sababu ya kuwapo kwa idadi kubwa ya majeruhi hao wa ajali ni kuongezeka kwa matumizi ya usafiri wa bodaboda nchini, kunakoiongezea Wizara ya Afya mzigo wa kutoa matibabu.

Ummy alisema mafunzo hayo yamekuja kwa wakati kwa sababu kumekuwapo na ongezeko la wagonjwa wanaotakiwa kufanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo, mishipa ya fahamu na ubongo na magonjwa mengine yanayohusiana na mashipa ya fahamu.

"Nimetolea mfano kuwapo kwa ongezeko la usafiri wa bodaboda umesaidia kuongeza upatikaniji wa usafiri maeneo ya mijini na vijijini lakini kwetu sisi sekta ya afya umetuongezea mzigo wa wagonjwa," alisema Ummy.

Alisema wengi wa majeruhi wa ajali ni vijana kuanzia 20 hadi 45 ambao wanafanya biashara ya kuendesha bodaboda ili kujipatia kipato.

Alisema gharama inakuja kwenye matibabu ya wagonjwa hao wa ajali katika upasuaji ambao unagharimu hadi Sh. milioni mbili kwa mgonjwa mmoja.

"Kwa hiyo huu usafiri wa bodaboda kwetu sekta ya afya umeleta mzigo. Sisi kama sekta ya afya tutajitahidi kuhakikisha yoyote atakayefika hospitali kwa sababu amepata majeraha atapatiwa huduma lakini nimesema ipo haja kama wizara kuzungumza na Wizara ya Mambo ya Ndani ili huu usafiri usimamiwe," alisema Ummy.

Alifafanua kuwa Taifa linatengeneza watu wengi wenye ulemavu kutokana ajali za usafiri wa pikipiki.

"Nilikuwa Arusha nimegawa miguu bandia kama 117 kati ya watano niliowapa miguu bandia ni vijana walipata ajali kutokana na usafiri wa bodaboda," alisema Ummy.

Aidha, alitoa rai kwa Watanzania wanaotumia usafiri huo, kuangalia usalama wao kwa kuzingatia ubora wa chombo na dereva.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Respicious Boniface, alisema maeneo makubwa wanayoumia majeruhi hao ni mshipa mkubwa wa mguu, kichwani na uti wa mgongo.

Kuhusu kumudu kuhudumia idadi hiyo, alisema wana wataalamu 10 ambao wanafanya kazi usiku na mchana kila siku kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofika MOI.

Dk. Boniface alisema wanavifaa vya kisasa vya kufanya upasuaji na kila siku wanafanya upasuaji ili kuondoa mrundikano wa wagonjwa wodini.

# Tanzania kuwa kitivo biashara ya mafuta EA

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo, kuanza ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta yanayowasili nchini na kuwa kitivo cha biashara hiyo ukanda wa Afrika Mashariki.

Imesema hatua hiyo inatokana na bei ya soko la dunia kwa bidhaa ya petroli na dizeli kupanda kila mara, hivyo uwezo wa kuhifadhi utaongeza uhakika wa uwepo bidhaa hiyo kwa kipindi kirefu.

Waziri wa Nishati, January Makamba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua mradi wa mabadiliko na kuhifadhi mazingira kwenye kituo cha mafuta TotalEnergies, maalum kwa ajili kuendesha shughuli zao kwa mfumo wa umeme wa jua.

Makamba alisema kwamba kupanda kwa bei hakuepukiki kutokana na soko lake kutegemeana na hali ya uchumi duniani, akisema sababu ya ongezeko la petroli na dizeli nchini hivi sasa kumetokana na vita inayoendelea Ukraine.

"Serikali tumechukua hatua kwa kuondoa tozo katika mafuta, lakini bei itaendelea kupaa. Sasa serikali inajiandaa na bunge lijalo la bajeti ya wizara, itatangaza jitihada za kuhakikisha gharama hizi hazimwathiri Mtanzania. Uimara wa mafuta nchini kwetu ndio maana yake stability kwa nchi jirani.

"Sababu za kupanda kwa mafuta nchini zipo nje ya uwezo, hivyo lengo la kukabiliana na hilo ni kujenga kituo kikubwa cha upakuaji mafuta nchini. Tunatarajia kuwa kituo kikubwa cha uhifadhi mafuta bandarini ya Dar es Salaam, ni wazi kuwa miundombinu ya sasa kutokidhi," alisema Makamba.

Alisema Bandari ya Dar es Salaam, si tegemeo pekee kwa nchi kwa kuingiza bidhaa tofauti kutoka nje bali uwapo wake ni hakikisho la shughuli za nchi jirani, akisema hivi asilimia 40 ya mafuta yanayoingia nchini kupitia bandari hiyo yanakwenda kwa majirani.

"Asilimia takribani 40 ya mafuta yaliyohifadhiwa Kurasini kupitia bandari yetu yanapita tu si ya kwetu. Tunalenga kuleta mapinduzi katika nishati. Mmekuwa 'first solarize fuel station' Tanzania, kuleta mabadiliko na kujizatiti katika utunzaji wa mazingira na kuunga mkono ndoto ya dunia kufikia 0 kaboni ifikapo 2050," alisema Makamba.

Alibainisha kwamba serikali itaendelea kuongeza hatua ili kuhakikisha nchi na nchi jirani zinapata mafuta kwa uhakika, akisema kwa kipindi cha miezi 17 bei imepanda mara mbili na kusababisha gharama za maisha kuongezeka.

Mkurugenzi Mtendaji wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Jean-Francois Schoepp, alisema kampuni hiyo imeshabadili vituo 24 kati 100, kuja kwenye mfumo wa umeme wa jua, na kwamba ifikapo mwishoni mwa mwaka huu vingine 68 vitafikiwa na mfumo huo.

"Tumelenga kutumia mfumo huu ili kutunza mazingira na kufanikisha malengo ya dunia ya kuwa na 'zero carbon' ifikapo mwaka 2050. Ili kufikia lengo hilo ukizingatia ongezeko la watu, miji, kupunguza hewa huwa ukaa ya kaboni ipo haja ya kuja na mbinu mpya," alisema Schoepp.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII - TASAF



SALAMU ZA PONGEZI

Kamati ya Taifa ya Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF
wanatoa pongezi kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
kwa kutimiza mwaka mmoja wa kuwa madarakani

*Pamoja Tuondoe Umaskini*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
S.L.P. 2719 Dodoma, Tanzania
**Simu:** +255 26 296 3866 **Nukushi:** +255 26 296 3871
**Tovuti:** www.tasaf.go.tz **Barua pepe:** info@tasaf.go.tz

# Jafo afunguka taharuki ripoti Mto Mara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amewataka wananchi kuepuka taharuki inayoendelea mitandaoni kuhusu ripoti ya uchafuzi wa Mto Mara huku akiagiza timu ya wataalamu wa ofisi hiyo, Wizara ya Maji, Mifugo na Uvuvi kuchambua kwa kina na kuiweka wazi kwa umma kwa lugha ya Kiswahili.

Pia amedokeza namna kamati ya kitaifa ilivyofika kwenye eneo la Mto Mara kuchunguza uchafuzi huo kwa kutumia helikopta ya jeshi. Alisema jana jijini hapo alipokuwa akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari baada ya kupokea ripoti ya kamati hiyo iliyokuwa ikiongozwa na Prof. Samwel Manyele wa Idara ya Uhandisi wa Kemikali na Madini kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Aliwataka Watanzania kuwa watulivu na kuepusha taharuki wakati serikali ikitimiza wajibu wake kwa kuwa azma ya serikali ni kulinda afya za wananchi wake na kwamba taarifa hiyo haikinzani na ya Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria.

"Nafahamu nimepitia mitandao nimeona kuna taharuki nyingi, niwaombe sana watu tuepuke taharuki wakati mwingine, wakati serikali inashughulikia haya mambo tunatakiwa kushughulikia kwa hekima kubwa sana sisi tuliunda timu tumepata taarifa na ripoti imepatikana," alisema.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Mary Maganga na wataalamu hao kuichakata ripoti hiyo na kuweka wazi kwa umma ili waisome.

"Wakati mwingine inawezekana kimepatikana kipande kidogo mistari miwili au mitatu yawezekana ufahamu ukawa nani, sasa wataalamu mzalishe hii ripoti kwa kadri mtakavyoona inafaa na muitafsiri kwa lugha rahisi na ya Kiswahili ili kila mtu asome kwa ajili ya faida ya leo na kesho," alisema.

Waziri Jafo aliwaomba Watanzania kusoma kwa kina ripoti hiyo ili kujua kilichoko kwa kuwa serikali imeunda hiyo timu kwa lengo la kupata faida.

"Tukiwa watulivu tutapata faida kubwa sana hasa mambo yaliyoelezwa kwenye ripoti hiyo mengi sana, nimeuliza wataalamu nimeona kuna ripoti ya Bonde wametoa takwimu hizi, nikauliza wataalamu wamesema yale yanayozungumzwa na bonde yote yamo isipokuwa hii imeenda kuangalia chanzo, suala la oksjeni kuwa chini ipo, suala la kuonekana kwa mafuta limeelezwa kiundani zaidi."

"Ripoti hii ina mambo yote humu ndani kwa hiyo kubwa zaidi wataalamu hakikisheni mnachambua, kuweka vizuri kuandaa mpango kazi wa jinsi gani tutatekeleza lakini vile vile watu wengi waipate ripoti hii haya ni maelekezo yangu waipate waisome, waone yaliyomo ndani yaliyoelekezwa humu kuna mambo mengi sana," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa kuna tatizo kubwa la mazingira nchini hasa magugu vamizi.

Aliongeza "Zile picha za video ukiangalia wataalamu wakati wanaruka na ndege Mto Mara ulivyo lile eneo oevu lilivyovamiwa inatupa mashaka siku za usoni tusipofanya haraka, nini kifanyike kwa haraka changamoto ya magugu maji imekuwa kubwa sana."

Alisema ripoti hiyo imebainisha tatizo la magugu maji, mifugo, shughuli za kibinadamu na mengine yameainishwa.



Mkuu wa Utawala Ofisi Ndogo ya Chama Cha Mapinduzi, Lumumba Mkoa wa Dar es Salaam, Christopher Ngubiagai (kulia), akipokea tuzo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa CCM, Grace Matoi, katika kongamano la kumpongeza Rais Samia kwa kutimiza mwaka mmoja kwenye uongozi wake, halfa iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HELSB kufanya mapitio mfumo ugharamiaji elimu

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Abdul-Razaq Badru, amesema ajenda kubwa ya HESLB kwa sasa ni kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa sasa wa ugharamiaji wa elimu ya juu ili kuakisi maoni ya wadau na hali ya sasa.

Badru aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizungumzia mafanikio ya Bodi hiyo katika mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika ofisi ya Azam TV mkoani Dar es Salaam.

"Tunafanya mapitio makubwa ya mwaka huu ya utaratibu wa sasa wa mikopo ya elimu ya juu ili kuwa na mfumo unaoakisi hali ya sasa na maoni ya wadau wetu ambao ni wabunge, wanafunzi, waajiri, wazazi, mamlaka ya ithibati na taasisi za elimu ya juu," alisema Badru.

Alisema mapitio hayo pia yataangalia gharama za fedha wanazotoa kama zinakidhi mahitaji na namna gani ya kuwahudumia ambao hawanufaiki kwa sasa.

Alisema maboresho hayo makubwa ya bodi hiyo pia yatalenga kunufaisha na vijana wa elimu ya kati ikiwamo elimu ya ufundi stadi ili kunufaika na mikopo hiyo.

Alitaja kundi lingine ni la wanafunzi wanaosoma nje ya nchi ambao wataandaliwa utaratibu wa kunufaika na mikopo hiyo inayotolewa na serikali. Akizungumzia mafanikio ya mwaka huo mmoja wa Rais Samia, alisema wamefanikiwa kuongeza bajeti ya mikopo kwa asilimia 23.

"Serikali ya wamu ya sita, imesaidia kuongeza bajeti ya mikopo na kufikia wanafunzi wengi zaidi sasa hivi tunakaribia Sh. bilioni 570," alisema Badru.

Kadhalika, alisema wamefanikiwa kujiunga na mfumo wa malipo kwa njia ya kidigitali, unaowezesha wanafunzi kupata mikopo haraka.

"Hili ni jambo lililokuwa kwenye mkwamo kwa muda mrefu na sasa umesaidia kupunguza usumbufu na kuongeza ufanisi kwa watendaji na wanafunzi kupata mikopo kwa wakati," alisema.

Pia wanaodaiwa na Bodi tarifa zao zimeingizwa kwenye mfumo wa mishahara, kwa watumishi wa umma watakatwa moja kwa moja.

"Awali haikuwezekana, sasa inawezekana mtu akikatwa mshahara wataona kwenye hati ya mshahara na inapunguza waajiri kufuatilia makato kwa watumishi wao," alisema.

# Amcharanga mapanga mume kisha kujinyonga

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MWANAMKE mkazi wa Kijiji cha Sibwesa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Wande Emmanuel (30), amemjeruhi mumewe, Dotto Enosi (35) kwa kumkata na panga kichwani kisha na yeye kujinyonga kwa kutumia kitenge.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame Hamad, alisema tukio hilo lilitokea Ijumaa, na chanzo ni ugomvi wa kifamilia unaohusiana na shughuli za kilimo.

Kamanda Hamad alisema mwanaume alikuwa akimtuhumu mkewe kwa kutoshiriki katika shughuli za kilimo, hivyo kusababisha ugomvi.

Alisema kutokana na ugomvi huo Wande aliamua kumkata kwa mapanga mumewe na kumjeruhi baada ya kugundua kuwa anaweza kufariki na yeye kutuhumiwa kwa kesi ya mauaji.

Alisema baada ya kumjeruhi, Wande alizunguka nyuma ya nyumba yao na kujinyonga.

Kamanda Hamad alisema Dotto alipelekwa Hospitali ya Rufani mkoani Katavi kwa ajili ya matibabu, na sasa hali yake inaendelea vizuri.

**Alisema kutokana na ugomvi huo Wande aliamua kumkata kwa mapanga mumewe na kumjeruhi baada ya kugundua kuwa anaweza kufariki na yeye kutuhumiwa kwa kesi ya mauaji.**

## HABARI KITAIFA

## Wasafirishaji kemikali wahimizwa chanjo UVIKO

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewahimiza madereva wanaosafirisha kemikali nchini na Watanzania wote kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kulinda afya zao na kuimarisha nguvu kazi ya taifa.

Dk. Mafumiko alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mafunzo ya madereva wanaosafirisha kemikali yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kupitia Ofisi ya Kanda ya Mashariki.

"Naunga mkono jitihada za serikali yetu katika kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 ulioenea kwenye nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania, hivyo ningependa niwasisitize na kuwahamasisha kuhusu kupata chanjo ya ugonjwa huu ambayo inatolewa bure na kwa hiyari katika vituo mbalimbali vya afya kote nchini," alisema Dk. Mafumiko.

Akiwasisitiza madereva kuhusu kuzingatia kanuni za usalama katika kusafirisha kemikali, alieleza kuwa pamoja na faida nyingi za kemikali katika maisha ya kila siku, ndani yake zimebeba hali hatarishi na zinaweza kuleta madhara makubwa kwa afya na mazingira kama zitatumika bila kuzingatia matumizi sahihi na usalama wakati wa uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi na matumizi mengine.

Akifunga mafunzo hayo Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai wa GCLA, David Elias, aliwataka madereva hao kujiepusha na utumiaji wa vilevi na dawa za kulevya kwa kuwa jambo hilo ni hatari katika usafirishaji wa kemikali.

"Ni matarajio yangu kuwa, baada ya mafunzo haya mtaweza kuzingatia taratibu za usafirishaji salama wa kemikali kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2020 katika nyanja zote.

Aidha, mnategemewa kuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha wadau na madereva wengi zaidi kupata mafunzo haya pamoja na kueneza elimu hii katika maeneo yenu ya kazi ili kulinda afya za watu, wanyama na mazingira," alisema Elias.

# Balozi Uingereza azungumzia mwaka mmoja wa Rais Samia

**Na Richard Makore, MWANZA**

BALOZI wa Uingereza nchini, amesifu uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia demokrasia hapa nchini ikiwa ni mwaka mmoja tangu aingie madarakani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Mwanza, Balozi David Concar, alisema nchi yake inaridhishwa na hali ya siasa inavyoendelea kwa sasa hapa nchini.

Alisema suala la kuwapo demokrasia limeimarika ndani ya mwaka mmoja na kwamba wataendelea kuunga mkono juhudi hizo.

Alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika nyanja mbalimbali za kiuchumi kwa manufaa ya nchi hizo mbili.

Aliongeza kuwa kwa sasa uhuru wa vyombo vya habari umeimarika ndani ya mwaka mmoja wa utawala wa Rais Samia, huku akishauri waandishi wa habari mkoani Mwanza (MPC) kuweka mpango kazi ili kuandika habari zinazohusu wanawake na watoto.

"Ni vyema MPC kwenye mpango kazi wenu ikaweka jukumu la kuripoti habari zinazohusu usawa wa kijinsia na haki za wanawake na watoto," alisema balozi huyo.

Kuhusu mzozo wa nchi za Ukraine na Urusi, alisema nchi itaendelea kujikita kutoa misaada ya kibinadamu na inaamini kwamba uvamizi huo haukuwa wa haki.

Kutokana na hali hiyo, balozi Concar alisema mataifa mengi yalipaza sauti zao kupinga Urusi kuvamia Ukraine na kumtaka Rais Vladmir Putin kusitisha vita hiyo.

Kwa upande wao, baadhi ya waandishi wa habari mkoani Mwanza, walimshukuru, balozi huyo kwa nchi yake kuwa na programu maalum ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (katikati), akikata utepe katika hafla ya kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick Gold Corporation kupitia migodi yake ya dhahabu ya Bulyanhulu na Buzwagi kukabidhi mashine mbili za kupimia UVIKO- 19 kwa Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Korti yabariki adhabu miaka 20 jela waliokutwa na nyara

**NA Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania, Kanda ya Mtwara imetupilia mbali rufani iliyokatwa na wafanyabiashara wawili na kuamuru watumikie adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela kwa kujihusisha na biashara ya meno ya tembo.

Hukumu hiyo ilitolewa mbele ya jopo la majaji watatu, Dk. Gerald Ndika, Rehema Kerefu na Penterin Kente baada ya kupitia hoja mbalimbali za rufani zilizowasilishwa na warufani Chande Ngayaga na Mohammed Rupembe wakipinga adhabu waliyopewa.

Jopo likisoma hukumu hiyo lilisema warufani walishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi kwa tuhuma za kukutwa na nyara ya serikali ambayo ni jino moja la tembo lenye thamani ya Sh. milioni 31 bila kibali.

Washtakiwa walikana kuhusika na tukio hilo na baada ya kesi kusikilizwa Mahakama iliwatia hatiani na kuwapa adhabu ya kulipa faini Sh. milioni 63 wakishindwa waende jela miaka 20.

Mashahidi upande wa Jamhuri walikuwa watano na katika ushahidi nyara hiyo inadaiwa kukutwa katika pikipiki aina ya King Lion yenye namba ya usajili T. 839 CLA, pikipiki na nyara vyote vilipokelewa mahakamani kama kielelezo.

Shahidi wanne, Filipo Orio katika ushahidi wake alidai uzito wa jino hilo ni kilo 0.55, thamani yake Sh. milioni 31.5.

Filipo alitoa hati ya uthamini wa nyara hiyo na ilipokelewa kama kielelezo mahakamani na alidai warufani katika maelelezo yao ya onyo walikiri kuhusika katika biashara ya meno ya tembo.

Katika utetezi wao warufani walikana kuhusika na kudai wakati wanakamatwa hawakukutwa na kitu mikononi, pikipiki na nyara pia havikuwapo.

Wanadai katika maelezo ya onyo walikubali taarifa zao binafsi tu lakini taarifa zote kuhusu biashara ya meno ya tembo walikana.

Mahakama ya chini wakati inatoa hukumu ilizingatia maelezo ya onyo ya washtakiwa ambayo walikiri kuhusika na biashara ya meno ya tembo.

Mahakama iliwatia hatiani na kuwapa adhabu ambayo walipinga Mahakama Kuu ambapo ilitupwa.

Warufani walihamia Mahakama ya Rufani kupinga hukumu ya Mahakama ya chini wakiwa na sababu tano.

Miongoni mwa sababu hizo ni kwamba Jamhuri haikuthibitisha mashtaka dhidi yao pasi na kuacha shaka.

Walidai maelezo ya onyo yalichukuliwa kinyume na utaratibu, Jamhuri walishindwa kutoa mahakamani hati ya ukamataji.

Jopo la majaji baada ya kupitia hoja hizo na majibu ya Wakili wa Serikali Mwandamizi, Faraja George aliyepinga hoja za warufani kwa madai kwamba hazina msingi, Jamhuri walithibitisha mashtaka dhidi yao lilikubaliana na hoja za Jamhuri.

"Warufani ni mashahidi wazuri kupitia maelezo yao ya onyo, mahakama inakubaliana na hoja za Wakili George kwamba malalamiko kuwa Jamhuri hawakuonyesha mnyororo wa ushahidi na kwamba mashahidi walijichanganya hayana msingi.

"Sababu zote tano za rufani hazina msingi, mahakama imepitia ushahidi kwa ujumla wake, hakuna shaka kwamba warufani walikutwa na nyara ya serikali," lilisema jopo.

Baada ya kusema hayo mahakama ilitupilia mbali rufani na kuamuru warufani kutumikia kifungo cha miaka 20 jela.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkakati uwepo upatikanaji wa maji maeneo ya vijijini

**MAJI** ni hitaji muhimu sana katika maisha ya binadamu. Kutokana na umuhimu huo, kuna usemi kuwa 'bila maji hakuna uhai'.

Maji yanahitajika kwa ajili ya kupikia, kunywa, kufulia, kumwagilia, viwandani pamoja na shughuli nyingine nyingi. Kukosekana kwa maji, kunasababisha shughuli nyingi kusimama, zikiwamo za nyumbani na uzalishaji mali.

Licha ya umuhimu wa maji, mahitaji ya maji katika maeneo mengi ya nchi yetu ni makubwa kuliko maji yanayozalishwa. Maeneo mengi ya vijijini yanaathirika zaidi kutokana na kutopata huduma ya majisafi na salama kulinganisha na mijini.

Hatua kadhaa zimekuwa zikichukuliwa na serikali katika kuhakikisha kwamba huduma ya majisafi na salama inapatikana kwa Watanzania wengi mijini na vijijini pamoja na mambo mengine, kuwawezesha wananchi kuwa na afya njema.

Kadhalika, mikakati mbalimbali imekuwa ikianzishwa na kutekelezwa kwa ajili ya kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za majisafi na salama katika maeneo ya vijijini, ambayo yamekuwa yakitoa kilio cha uhaba wa huduma hiyo kwa serikali.

Katika kuhakikisha kwamba wananchi wa vijijini wanapunguziwa kero hiyo, serikali inasema ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba maji ya uhakika yanapatikana katika maeneo ya vijijini.

Aliyebainisha dhamira hiyo ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegalo, na kuweka wazi malengo matatu yanayolenga kurahisisha upatikanaji wa maji vijijini ikiwamo kuanzisha mfumo mpya wa kusanifu miradi kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji.

Aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam katika mjadala maalumu wa kuonyesha mafanikio ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, na kubainisha kuwa watatumia vyanzo vikubwa kama maziwa kuhudumia vijiji vingi kwa wakati mmoja.

Mkakati wa pili alisema ni kupunguza gharama za maji vijijini ili yawe yapatikane kwa urahisi na watatu ni kuanzisha mfumo wa malipo kabla ya huduma na wanatarajia mwezi ujao kuingia makubaliano ya kimkataba na Chuo cha ufundi cha Arusha, Dar es Salaam na Mbeya ambao wameshawahakikishia kwamba wana uwezo wa kuandaa mifumo husika ambayo itatumika kirahisi na watu wa kijijini.

Alisema wanataka waunganishe na mifumo ya simu za mikononi ili mtu akiwa mjini anaweza kumnunulia maji mama yake kijijini akalipa akaenda kuchota maji kwa kutumia kadi.

Kwamba ndiyo maeneo ambayo wanataka kuyapa kipaumbele ili kupunguza gharama pamoja na kurahisisha upatikanaji wa maji vijijini. Pia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia wamepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini pamoja na kutekeleza miradi 522 na kupeleka maji kwenye vijiji vipya 1,560 ambavyo vimewezesha zaidi ya watu milioni mbili kupata huduma hiyo.


Tunaridhishwa na hatua za serikali kuongeza miradi ya maji na mikakati hii ya kupanua wigo wa upatikanaji maji vijijini, lakini tunashauri kwamba mipango na mikakati tunayoelezwa itekelezwe kwa vitendo, ili wananchi wetu waondolewe vikwazo katika suala zima la upatikanaji wa huduma ya maji.

Haitakuwa vizuri kubainisha mikakati mizuri, lakini mwishowe isitekelezwe kwa visingizio mbalimbali. Tunaamini kuwa mikakati aliyoieleza Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA itatekelezwa kwa kuwa fedha zitaliwa zimepatikana au zinakaribia kuiva.

Tunatarajia kusikia mikakati na mipango mingine mingi kutoka kwa watendaji wa mamlaka za maji nchi nzima na wa Wizara ya Maji wakati huu wa maadhimisho ya Wiki ya Maji kuhusiana na walivyojipanga kubuni na kuendeleza miradi iliyoko, kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa maji hususan katika maeneo ya vijijini.

Matumaini yetu yanatokana na serikali kuipatia RUWASA Sh. bilioni 79.5 ambapo wanatarajia kutekeleza miradi mingine kwenye vijiji 331 na kupitia vijiji hivyo wananchi zaidi ya milioni 1.36 watapata huduma ya maji, kupitia fedha za UVIKO-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kuifanyia ubadhirifu miradi ya elimu kunalikwamisha Taifa

**MGAWO** wa fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya jamii na mapambano ya UVIKO -19 zimetumika pia kujenga madarasa katika shule mbalimbali nchini na kupunguza uhaba wa madarasa uliokuwapo kwa muda mrefu.

Hatua hiyo ya kujenga madarasa mengi, imesaidia kuwafanya wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu kuanza masomo kwa pamoja, tofauti na miaka ya nyuma walipoianza kwa awamu.

Pamoja na juhudi hizo za serikali za kutaka kuinua elimu nchini, kumekuwapo tuhuma kwenye baadhi ya halmashauri kubainika kuwa na matumizi yasiyoridhisha ya fedha hizo.

Akiahirisha Mkutano wa Sita wa Bunge la 12 Bungeni jijini Dodoma, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisisitiza kuwa hatua kali zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wote wanaobainika kufanya ubadhirifu wa fedha hizo.

Kwamba, kutokana na taarifa za ubadhirifu mkubwa katika baadhi ya halmashauri, serikali itapeleka timu maalumu ya uchunguzi kujiridhisha na matumizi ya fedha za umma.

Amewataka wakuu wa mikoa kufanya ukaguzi wa kila mara kwenye matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha miradi inafikia hatua kuakisi thamani ya fedha za Watanzania.

Binafsi ninadhani ingekuwa vyema kama viongozi wanaotuhumiwa kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za umma, wazingatie kutotimia vyeo kwa manufaa yao badala yake viwe ni kwa ajili ya umma.

Kama anavyosema waziri, hizo ni fedha za umma na zinatolewa kwa ajili ya miradi ya umma, hivyo ni wajibu zikasimamiwa vyema ili kuboresha miradi iliyokusudiwa, ikiwamo ujenzi wa madarasa.

Ikumbukwe kwamba ni kwa muda mrefu, wanafunzi wa kidato cha kwanza walikuwa wakianza muhula wa masomo kwa awamu, kutokana na uhaba wa madarasa, lakini serikali imejitahidi kutafuta fedha ili kumaliza kero hiyo.

Ninaamini kuwa matarajio ya serikali ni kuhakikisha fedha hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa, ili kumaliza kero ya uhaba wa madarasa, zinajitokeza tuhuma za ubadhirifu wa fedha hizo inasikitisha.

Wiki chache zilizopita, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amebaini upotevu wa fedha na matumizi yasiyosahihi ya kiasi cha Sh. milioni 231.84.

Fedha hizo ni za ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kumbukumbu ya Sokoine, bwalo la chakula, miundombinu ya jiko na bweni na kumtaka Mkurugenzi wa halmashauri hiyo Hassan Njama, kutoa ufafanuzi wa fedha hizo.

Kwa mujibu wa Bashungwa, tathmini iliyofanywa na kamati maalum ya ukaguzi wa matumizi ya fedha za ukamilishaji wa miundombinu katika shule hiyo imebaini upotevu, matumizi yasiyo sahihi ya Sh. milioni 231.84.

Ingekuwa ni vyema kama kasi anayokwenda nayo Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha elimu, ingeungwa mkono na wasaidizi wake kuanzia ngazi zote ili aweze kufikia malengo aliyokusudia.

Ninashauri hivyo, kwa sababu zinapojitokeza tuhuma za ubadhirifu wa fedha za miradi mbalimbali, ni wazi hatua hiyo ni sawa na kumkwamisha, pia ni kuwakwamisha Watanzania wanaotamani kusonga mbele kielimu.

Ikumbukwe kuwa wanapojenga miundombinu isiyolingana kiasi cha fedha kilichokusudiwa, maana yake ni kuiingiza serikali kwenye gharama nyingine ya kutafuta fedha nyingine bila kutarajiwa.

Waliopewa majukumu ya kuwatumikia Watanzania katika ngazi mbalimbali, ni vyema wakasimamia kikamilifu miradi yote ya umma kwa manufaa ya nchi na watu wake na siyo kwa manufaa ya wachache.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA

"WIKI YA MAJI 2022"

# MAENDELEO KATIKA SEKTA YA MAJI TANGA

**UTANGULIZI**
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) ni Mamlaka iliyoanzishwa mnamo mwaka 1998 na inafanya kazi kwa mujibu wa sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2019.

Tanga UWASA inazalisha na kusambaza majisafi na salama kwa wateja wake na kutoa huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka kwenye maeneo ya wateja. Wastani wa uzalishaji na usambazaji wa majisafi unafikia kiasi cha mita za ujazo 30,000 kwa siku kukidhi asilimia 90 ya mahitaji ya wakazi wa eneo la huduma ambalo linajumuisha Jiji la Tanga na Miji ya Muheza na Pangani wanaofikia 378,028.

Vyanzo vya maji vinavyotumiwa na Tanga UWASA ni Bwawa la Mabayani linalopokea maji kutoka katika Mto Zigi lenye uwezo wa kuhifadhi meta za ujazo milioni 7.7, Mto Mkurumuzi na visima 12.

Tanga UWASA inatoa huduma ya uondoshaji wa majitaka yanayozalishwa kutoka katika maeneo mbalimbali ya wateja wake kwa kutumia mtandao wa mabomba na gari maalum la uondoshaji majitaka. Mtandao wa huduma ya majitaka unatoa huduma kwa asilimia 7.41 ya wakazi wa Jiji la Tanga pekee na maeneo yaliyobaki yanapatiwa huduma kwa kutumia gari la uondoshaji wa majitaka

**MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI DUNIANI 2022**
Wizara ya Maji ilizindua rasmi maadhimisho ya Wiki ya Maji kitaifa tarehe 15/03/2022 huko Orkasumet, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara; ambapo pia liliwekwa Jiwe la Msingi kwenye mradi mkubwa wa Maji wa Orkasumet. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kilele chake ni tarehe 22/03/2022.
Maadhimisho hayo kwa mwaka huu 2022 kitaifa yana kauli mbiu isemayo "MAJI CHINI YA ARDHI - HAZINA ISIYOONEKANA KWA MAENDELEO ENDELEVU", ambapo Kauli mbiu kwa Kimataifa inasema "GROUNDWATER, INVISIBLE TREASURE FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT". Maadhimisho ya mwaka huu pia yanaenda sambamba na kumbukumbu ya mwaka mmoja madarakani wa Mhe. SamiaSuluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Katika maadhimisho haya, Tanga UWASA inajitathmini katika maeneo yafuatayo: -

**A. HALI YA UPATIKANAJI HUDUMA**

Tanga UWASA inahudumia wakazi wapatao 378,028 walioko katika Jiji la Tanga pamoja na miji ya Pangani na Muheza. Huduma ya Majisafi kwa ujumla inawafikia wakazi wapatao 340,225 sawa na wastani wa asilimia 90 na kwa upande wa huduma ya Majitaka inafanywa kupitia mtandao uliojengwa katika Jiji la Tanga pekee na unawafikia wakazi wapato 23,718 sawa na asilimia 7.4.
Mamlaka inaendelea kutekeleza ujenzi wa miradi mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za usambazaji Majisafi na uondoshaji wa Majitaka katika maeneo ya utoaji wa huduma ili kufikia malengo yaliyopo katika Ilani ya Chama Tawala kwa utoaji wa huduma ya majisafi Maeneo ya mjini kufikia wastani wa asilimia 95 na kuboresha huduma ya uondoshaji Majitaka.

B. **MIRADI INAYOTEKELEZWA NATAASISI**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) kati ya mwezi Machi Mwaka 2021 na sasa, inatekeleza jumla ya miradi10 yenye lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma za Majisafi pamoja na uondoshaji wa Majitaka katika maeneo yake ya utoaji wa huduma (Jijini Tanga, na miji ya Pangani na Muheza). Miradi hii inayoendelea kutekelezwa imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji, na inathamani jumla ya TZS 22,221,342,314.

**C. HUDUMA YA MAJISAFI KWA KAYA ZISIZO NA UWEZO (SERVICE TO URBAN POOR).**

Katika utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002, Tanga UWASA inatoa huduma ya Majisafi bure kwa kaya zipatazo 71 zilizopo Jijini Tanga. Tathimini ya watu wenye sifa za kupata huduma ya Majisafi bure inaendelea kufanyika katika maeneo yote ya huduma ikiwemo miji ya Pangani na Muheza ili hatimaye huduma hii ipatikane kwa wakazi wa maeneo yote ya huduma.

**D. UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI**
Vyanzo vya maji kwa maeneo ya huduma ya Tanga UWASA vipo chini ya Bonde la Mto Pangani ambapo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) kwa kushirikiana na Bodi ya Bonde la Mto Pangani, wanafanya jitihada kubwa za kuwezesha uhifadhi wa mazingira katika vyanzo vyake vya maji.
Tanga UWASA imeendelea kushirikiana na Umoja wa Wakulima Wahifadhi Mazingira Kihuhwi Zigi (UWAMAKIZI) kufanya miradi na shughuli mbalimbali zenye kulenga kuhifadhi mazingira katika maeneo ya chanzo cha Mto Zigi. Umoja huo kwa sasa una wanachama wapato 1,540 waliopo katika vijiji 17 vya Wilaya ya Muheza na Kijiji kimoja kilichopo Wilaya ya Mkinga.
Lengo la Umoja huu ni kuwahamasisha wananchi waishio maeneo ya vyanzo vya Maji kujishughulisha na miradi na kazi mbalimbali zinazoweza kuwapatia kipato bila kuathiri mazingira na vyanzo vya maji kwa ujumla. Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, ufugaji, kupanda miti pamoja na biashara ya mazao ya kilimo na miti.
Jitihada hizi zimepelekea kuendelea kuwepo kwa maji yanayo tiririka katika mto Zigi na mto Kihuhwi iliyopo katika misitu ya Amani ambayo maji yake huingia katika bwawa la Mabayani ambalo ndiyo chanzo tegemezi cha maji kwa wakazi wa Jiji la Tanga na Mji wa Muheza kwa sasa.

**TAARIFA YA MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KATIKA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA SITA.**
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) kati ya mwezi Machi Mwaka 2021 hadi sasa inatekeleza jumla ya miradi10 yenye lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma za Majisafi pamoja na uondoshaji wa Majitaka katika maeneo yake ya utoaji wa huduma kama ifuatavyo;

**1: MRADI WA KUBORESHA HALI YA UPATIKANAJI WA MAJI TANGA AWAMU YA II**
Ujenzi wa mradi ulianza mwezi Agosti 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022 ambapo kwa sasa mradi huu umefikia asiliamia 40 ya utekelezaji wake katika eneo la Pande Jijini Tanga ambao unagharimu kiasi cha shilingi 9,180,580,873.
Kazi zilizokusudiwa kufanyika ni Ulazaji wa bomba kubwa lenye kipenyo cha 600mm kutoka Mowe hadi Kange na urefu wa km 12.4, Ujenzi wa Tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 1,000 na Kukarabati na kuongezea uwezo wa uzalishaji mtambo wa kusafisha na kutibu maji Mowe.
Manufaa ya mradi yanalenga kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Jiji la Tanga na miji jirani ya Kasera mkinga na Muheza pia mradi huu utawezesha wakazi wa Tanga wapatao 382,095 kupata maji masaa 24 kwa siku kutoka wastani wa masaa 21 kwa siku.

**2: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KUPITIA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19**
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) inatekeleza mradi wa Uendelezaji Mtandao wa Mabomba Jijini Tanga kupitia fedha za UVIKO - 19 wenye thamani ya shilingi 555,721,250, Ambazo zimetengwa na Wizara ambapo kazi zilizokusudiwa kufanyika ni kuendeleza mtandao wa mabomba wenye urefu wa km.17.8 ili kuwafikia wakazi wa maeneo ya Maweni, Pongwe, Kichangani, Neema na Mwahako
Mamlaka inatekeleza mradi huu wenye lengo la kusogeza huduma ya maji kuwafikia wakazi wa maeneo tajwa wapatao 7200 na mpaka sasa umefikia asilimia 40 ya utekelezwaji. Ujenzi wa mradi umeanza Desemba 2021 na unatarajiwa kukamilika Mwezi April 2022.

**3: UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KUBORESHA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI MAENEO YA MPIRANI, NDAOYA, KIBAFUTA, MLENI NA CHONGOLEANI**
Mradi una gharama ya shilingi 918,541,688.00, ambapo kazi zilizokusudiwa kufanyika ni ulazaji wa bomba lenye urefu wa km 25,780, ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 225,000 na maunganisho ya Maji kwenye vituo 22 vya kuchotea maji. Vituo 19 vilivyounganishwa na mtandao wa maji vime shaanza kutoa huduma.
Mradi umefikia asilimia 90 ya utekelezaji wake na utakamilika Mwezi Aprili 2022, ambapo kukamilika kwake kutasaidia wakazi wa mitaa tajwa wapatao 15,750 kupata huduma ya majisafi..

**4: UJENZI WA BOMBA LA MAJI LENYE KIPENYO CHA DN300 NA UREFU WA MITA 8200 KUTOKA MOWE HADI PONGWE.**
Mradi unagharama ya shilingi 2,607,377,883.50 ambapo kazi zilizokusudiwa kutekelezwa ni ulazaji wa bomba la maji lenye kipenyo cha DN300 kutoka Mowe hadi Pongwe na urefu wa mita 8200. Mradi umekamilika mwezi Desemba 2021 kwa asilimia 100 na kwa sasa unatoa huduma kwa wakazi wa Kata za Mlingano, Ngomeni, Lusanga, Mpapayu na Genge wapatao zaidi ya 10,000.

**5: UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJISAFI MJI WA MUHEZA**
Ujenzi wa Miundombinu ya majisafi mji wa Muheza eneo la Muheza Mjini una gharama ya shilinngi 700,000,000, ambapo kazi zinazokusudiwa kuetekelezwa ni Uendelezaji wa mtandao wa mabomba ya majisafi katika mitaa ya Kwemkabala na Masuguru, Pamoja na kufanya ukarabati wa mfumo wa mabomba eneo la Muheza mjini kwa kubadilisha mabomba ya zamani na kulaza mapya.
Mkandarasi wa ujenzi pamoja na mzabuni wa kuleta mabomba na viungio wameshapatikana. Ujenzi utaanza Mwezi Machi 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022. Mradi huu utaboresha upatikanaji wa maji kutoka masaa 6 kwa siku hadi kufikia masaa 12 kwa siku., ambapo wakazi wa Muheza mjini wapatao 15,700 watafaidika na mradi huu.

**6: UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJISAFI MJI WA PANGANI**
Ujenzi wa Miundombinu ya majisafi mji wa Pangani eneo la Pangani Mjini una thamani ya shilingi 1,000,000,000 ambapo kazi zinazokusudiwa kufanyika ni Uendelezaji wa mtandao wa mabomba ya majisafi mitaa ya madanga, Kimang'a, Miembeni, na Choba, kufanya ukarabati wa mfumo wa mabomba eneo la Pangani Mjini sambamba kwa kubadilisha mabomba ya zamani na kulaza mapya Pamoja na Kuchimba kisima kipya na kufunga pampu ya maji



*Wajumbe wa Bodi ya Tanga UWASA katika ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inayosimamiwa na taasisi, Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tanga UWASA Dr. Fungo A.Fungo.*

eneo la Boza.
Mkandarasi wa ujenzi pamoja na mzabuni wa kuleta mabomba Pamoja na viungio wameshapatikana. Ujenzi utaanza Mwezi Machi 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022. Mradi huu utaboresha upatikanaji wa maji kutoka masaa 6 kwa siku kufikia masaa 12 kwa siku ambapo wakazi wa Pangani mjini wapatao 37,109 watafaidika na mradi huu.



*Kazi ya Ulazaji wa bomba kubwa lenye kipenyo cha 600mm na urefu wa Km 12.4 kutoka Mowe hadi Kange katika Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Tanga na Muheza Awamu ya Pili*

**7: UJENZI WA MABWAWA YA KUKUSANYA NA KUSAFISHA MAJITAKA MUHEZA**
Mradi una gharama ya shilingi 1,000,000,000, ambapo kazi zinazokusudiwa kufanyika ni Ujenzi wa mfumo wa kukusanya na kusafisha majitaka kutoka katika makazi ya watu kwani kwa sasa katika Mji wa Muheza haukua na mfumo wa majitaka kabisa. Hivyo kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 Serikali imewezesha ujenzi wa mfumo wa kukusanya, kutibu na kusafisha majitaka ikiwa ni pamoja na kununua magari ya kukusanya majitaka toka kwa wakazi wa Muheza na maeneo jirani.
Pia mfumo huo utanufaisha wakazi wote wa Muheza na maeneo jirani wapatao 37,109, ambapo Mzabuni wa ujenzi ameshakabidhiwa eneo la ujenzi na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022.

**8: UJENZI WA MABWAWA YA KUKUSANYA NA KUSAFISHA MAJITAKA PANGANI**
Mradi unahusisha Ujenzi wa mabwawa ya kukusanya na kusafisha Majitaka katika eneo la Pangani Mjini na una thamani ya shilingi 1,000,000,000, ambapo kazi zinazokusudiwa kufanyika ni Ujenzi wa mfumo wa kukusanya na kusafisha majitaka kutoka kwa wakazi wa Pangani. Mjini pamoja na kununua magari ya kukusanya majitaka toka kwa wakazi wa Pangani. Mradi huo utanufaisha wakazi wote wa Pangani na maeneo jirani wapatao 20,400.
Mzabuni wa ujenzi ameshakabidhiwa eneo la ujenzi na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022.

**9: MRADI WA USANIFU NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJITAKA JIJINI TANGA**
Mradi una thamani ya shilingi 4,855,120,620 ambapo kazi zinazokusudiwa kutekelezwa ni kufanya usanifu wa ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka na Usimamizi wa ujenzi wa mradi. Miundombinu ya Majitaka iliyopo imejengwa miaka zaidi ya 60 iliyopita na hivyo imechakaa na kuhitaji ukarabati mkubwa. Usanifu utasaidia kujua mahitaji na gharama halisi za mradi, ambapo Mhandisi Mshauri WAPCOS Co. Ltd ameshaanza kazi ya usanifu tangu Januari 2022 na anatarajia kumaliza mwezi Juni 2022.

**10: KUANDAA TAARIFA YA UDHIBITI WA ATHARI YA MAZINGIRA NA JAMII WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJITAKA**
Mradi una thamani ya shilingi 404,000,000 ambapo kazi zinazokusudiwa kuetekelezwa ni kupata taarifa ya kudhibiti athari ya Mazingira na Jamii. Ambapo Mhandisi Mshauri TANSHEQ Co. Ltd ameshaanza kazi ya kutafiti na hatimaye kuandaa taarifa ya athari katika jamii na mazingira na namna ya kudhibiti athari zitakazojitokeza wakati wa ujenzi wa mradi.
Kwa hiyo kwa ujumla Miradi hii inayoendelea kutekelezwa imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji, na kwa ujumla inathamani ya TZS 22,221,342,314.

**HITIMISHO**
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) katika utimizaji wa majukumu yake inalenga kutoa huduma bora ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa wakazi wa Jiji la Tanga pamoja na Miji ya Muheza na Pangani kwa njia inayokubalika kimazingira na kwa kutumia watumishi wenye ari ya kazi na kumjali mteja.



*Kazi ya Ujenzi wa Machujio katika Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Tanga na Muheza Awamu ya Pili.*



*Sehemu ya Matenki ya kuhifadhia maji katika Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya maji kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji maeneo ya mpirani, ndaoya, kibafuta, mleni na chongoleani.*

# TBS yaonya matairi ya magari yanayoagizwa nje

Na Sabato Kasika

IMEELEZWA kuwa asilimia kubwa ya magari yanayoingizwa nchini yana matairi ambayo hayafai kutumika, lakini baadhi ya wamiliki wake huwa wanaahidi wanapoelekezwa kuyabadili kwa ajili ya usalama wao.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani Dar es Salaam jana na Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Msasalaga, katika mkutano wa viongozi wa shirika hilo na wahariri wa vyombo vya habari.

Mkurugenzi huyo alisema, tairi imeandikwa tarehe ya kuisha muda wake, na kwamba magari mengi yanayoingizwa nchini huwa yana matairi ambayo muda wake umeisha, hali ambayo ni hatari kwa wamiliki wake.

"Hata kama haijatumika, iwapo imekaa hadi muda wake ukaisha, haifai kutumika tena, lakini bahati mbaya baadhi ya watu wanapenda njia ya mkato ili kuendelea kutumia matairi yaliyoisha muda wake," alisema Msasalaga.

Alisema matairi ndiyo gari na kwamba anashangaa kuona mtu ananunua gari ya bei kubwa halafu anashindwa kununua matairi badala yake anatafuta njia nyingine za mkato ambazo si salama kwao.

"Pale bandarini, taratibu zote za forodha zinafuatwa, kwani magari yote yakiwamo yenye matatizo hutolewa, lakini yenye matatizo wamiliki wake hutakiwa kwenda kufanya marekebisho na kurudi kutoa taarifa," alisema.

Alisema baadhi yao badala ya kurekebisha na kurudi kutoa taarifa, huwa wanatafuta njia nyingine ili kuendelea kutumia matairi ambayo yameisha muda wake na TBS iko makini na watu wa aina hiyo.

Meneja Upimaji, Joseph Makene, alisema, shirika hilo liko mbioni kuweka mitambo ya maabara kwenye kanda zake nne ikiwa ni njia mojawapo ya TBS kusogeza huduma zake karibu na wananchi.

Meneja huyo alitaja maeneo ambayo TBS inataka kuweka maabara zake kwa ajili ya kusogeza huduma za upimaji karibu na wananchi kuwa ni Mwanza, Kigoma, Dodoma, Mtwara, Mbeya, Arusha.

Meneja Viwango wa shirika hilo, Yona Afrika, alisema, viwango vina faida ikiwamo kuweka usawa katika uwanja wa biashara, kuondoa mkanganyiko kuhusiana na bidhaa na kusaidia kufungua masoko zaidi.

"Viwango urahisisha biashara kati ya nchi na nchi, hutoa uhakikisho wa ubora, usalama kuaminika na ufanisi na huipa serikali urahisi wa kuunda sheria zinazohusiana na masuala ya afya na usalama wa watumiaji wa bidhaa mbalimbali," alisema Afrika.




Meneja Upimaji wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Joseph Makene, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika mkutano ulioandaliwa na shirika hilo kwa ajili ya wahariri wa vyombo vya habari kuelezea jinsi linavyotekeleza majukumu yake. **SABATO KASIKA**

## TANROADS yaagizwa kukamilisha daraja Kitengule

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

WAKALA wa Barabara nchini (TANROADS), mkoani Kagera, wametakiwa kukamilisha kwa wakati ujenzi wa daraja la Kitengule ili kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa wilaya za Karagwe na Missenyi, mkoani Kagera.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Seleman Kakoso, alisema hayo jana akiwa na wajumbe wa kamati yake walipotembelea daraja hilo linalounganisha wilaya hizo.

Meneja wa TANROADS mkoani Kagera, Yudas Msangi, alisema, ujenzi huo ulioanza Oktoba mwaka 2018, unatarajia kukamilika Mei, mwaka huu.

Msangi alisema katika daraja hilo kuna barabara unganishi na ujenzi wake umefikia asilimia 36.8.

Alisema mradi huo upo nyuma kwa asilimia 2.92 kutokana na matatizo yaliyochelewa kuundwa kwa hati ya msamaha, kuondolewa ongezeko la thamani na mvua kuonyesha juu ya wastani.

Naibu wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alisema mwezi uliopita waziri wake, Profesa Makame Mbarawa, alipita katika barabara unganishi na daraja hilo na kuagiza zijengwe kwa kiwango cha lami na kazi hiyo imefikia asilimia 80.

Wakati huo huo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imetakiwa kuangalia upungufu kwenye viwanja vya Bukoba na Mwanza ili kuweka huduma bora na usalama wa abiria kuwalinda wanapoingia na kutoka.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliyasema hayo jana wakati akikagua uwanja huo na kuagiza kuwekwa taa za kuongoza ndege.

Aliagiza pia kufungwa vifaa vya kuzuia ndege wanaoruka au kusogeza karibu na uwanja kutokana na kuingilia mifumo na kusababisha madhara.

"Tatizo lililoko hapa ndilo lililoko hata Mwanza na wenyewe hawana taa, hivyo mamlaka wanajukumu la kuangalia upungufu huo na kuweka taa kwa ajili ya usalama wa abiria wanaotua na kuondoka," alisema Mwakibete.

Kaimu Meneja wa uwanja huo, Cecilia Kamwele, alisema licha ya kuwa na uwanja mdogo, eneo hilo lilifanyiwa ukarabati na upanuzi mwaka 2014 hadi 2017.

Vile vile, hivi sasa uwanja huo unachukua abiria 110 wanaowasili na kuondoka na tatizo lililoko ni kuwa jirani na Ziwa Victoria, shule, kituo cha afya na makazi ya watu.

# Wanaotiririsha kinyesi Mto Kizinga wapewa siku 7

Na Frank Monyo

BODI ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imetoa wiki moja kwa wafugaji wote wanaotiririsha kinyesi na mikojo ya mifugo katika Mto Kizinga ulioko Mtaa wa Mashine ya Maji Kata ya Buza Wilaya Temeke kuondoa mazizi yalioko ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo hicho.

Aidha, imetoa wiki mbili kwa wakazi wa eneo hilo kujenga vyoo imara kwa utaratibu wa kiafya na kuacha mara moja tabia ya kutiririsha maji ya choo katika mto huo na watakaokahidi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Akizungumza na wakazi wa eneo hilo jana katika maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo kilele chake ni leo, Ofisa wa Bonde la Wami/Ruvu ofisi ya Dar es Salaam, Halima Faraji, alisema kumekuwa na uchafuzi wa maji huo unaofanywa na wafugaji wa eneo hilo kwa kujenga mazizi kando ya mto, kutupa takataka na kutiririsha maji ya choo katika mto huo.

"Tumeona kuna watu ambao wameelekeza vyoo vyao kwenye mto huu, huu ni uchafuzi wa maji, wengine wamejenga mazizi ndani ya mita 60 kutoka mtoni, huu ni uharibifu wa rasilimali za maji na hatuwezi kuuvumilia, haya maji yanatumika na wananchi wengi hivyo tumetoa wiki moja kwa wafugaji pamoja na wiki mbili kwa wakazi wa eneo hilo kujenga vyoo imara na kuacha kutiririsha maji machafu katika mto huu," alisema.

Aliongeza kuwa kazi ya bonde ni kusimamia upatikanaji wa maji kwenye vyanzo na kusimamia ubora wa maji na kuhakikisha maji yanayopatikana yanakuwa safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

"Hapa kuna mitambo ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazigira Dar es Salaam (DAWASA) wanatumia gharama kubwa sana kutibu haya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Jumatatu (Machi 28) Bonde la Wami/Ruvu tutakuwa hapa kama tukikuta hii mifugo bado haijatolewa ndani ya mita 60 hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kutaifisha mifugo hii," alisema.

Ofisa Mazingira Wilaya ya Temeke, Dominick Saramba, alisema watahakikisha maagizo yote yaliotolewa yanaenda kusimamiwa kwa ajili ya kutunza mazingira pamoja na Rasilimali za Maji kwani katika zoezi hilo wameshirikishwa viongozi wa serikali za mitaa, DAWASA na halmashauri.

HABARI KITAIFA

## Vodacom, Eutelsat kujitanua maeneo ambayo hayajafikika

**Na Mwandishi Wetu**

VODACOM Tanzania, imetangaza kutia saini mkataba na Shirika la Eutelsat Communications ambao utawezesha kuunganisha huduma kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao wa kidijitali mikoani kupitia satelaiti yenye kasi kubwa ya Eutelsat KONNECT.

Huduma hii mpya itatoa fursa kwa wafanyabiashara binafsi na wa kimataifa, sekta ya utalii na hoteli ambapo mafanikio yameonekana katika majaribio yaliyofanikiwa kwa Vodacom Tanzania PLC kupanua wigo wa upatikanaji huduma na kuwafikia watumiaji ambao walikuwa hawajafikiwa awali. Huduma hizi zitatolewa na Vodacom huku vifaa vikiunganishwa na Konnect Africa.

Akizungumza wakati wa kutangaza mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Sitholizwe Mdlalose, alisema: "Tuna furaha kubwa kujumuisha huduma zetu kwenye satelaiti hii, tukitumia uwezo wa satelaiti mpya kabisa ya EUTELSAT KONNECT ambayo itatuwezesha kutimiza dhamira yetu ya kufikisha huduma za mtandao katika maeneo yote nchini."

Aliongeza kuwa kwa kutumia KONNECT, Vodacom itapanua mtandao wake kufikia asilimia 100 ya eneo lote la Tanzania, yaani kuunganisha mikoa na wilaya zote na vijiji bila kujali umbali husika. "Kwa huduma hii, tutaunganisha kila mtu, hii ni pamoja na maeneo ambayo hayajafikiwa hivi sasa, ikiwa na kasi ya hadi 100Mbps," alisema mkurugenzi huyo.

Alifafanua kuwa huduma hii inaendana na dhamira ya Vodacom Tanzania kuboresha upatikanaji wa huduma za kidijitali zenye kasi kwa watu wengi zaidi nchini kwa kubuni njia mpya za kufikisha huduma kwa watumiaji wote.

Akizungumza kwenye makubaliano hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Konnect Africa, Philippe Baudrier, alisema: "Tuna furaha kubwa kushirikiana na Vodacom Tanzania, kwa kupanua wigo wa mtandao wake Tanzania. Mkataba huu unaonyesha jinsi ambavyo uwezo mkubwa wa satelaiti ya EUTELSAT KONNECT unaweza kutimiza mahitaji makubwa kwa maeneo ya Bara la Afrika ambayo hayajafikiwa au yenye huduma hafifu, na ina ashiria mafanikio katika maendeleo ya usambazaji wa huduma baada ya makubaliano yetu nchini Nigeria, Afrika Kusini na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)."

# Takwimu mazingira sasa zafikia vigezo kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

KWA mara ya kwanza Tanzania imefanikiwa kutoa takwimu za kimazingira zinazokidhi vigezo vya kimataifa ambazo zinasaidia kufanya tathmini na utekelezaji wa miradi ya mazingira nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii kutoka ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, ndiye aliyethibitisha hatua hiyo alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya taasisi hiyo kwa mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu.

"Lakini tumefanya utafiti wa kimazingira, ambapo kwa mara ya kwanza Tanzania tumetoa takwimu ambazo zinakidhi vigezo vya kimataifa na tunaendelea kuboresha takwimu hizo ambazo zilikuwa 'zinagape' kubwa," alisema Ruth.

Alisema matokeo ya utafiti huo yamesaidia kufanya maboresho, kutunza fedha na kutathmini utekelezaji wa maendeleo ya nchi yetu katika muktadha wa kimazingira.

Alisema taasisi hiyo pia imeendelea kuzalisha takwimu zake za msingi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Tumeendelea kutoa taarifa ya mfumuko wa bei kwa kila mwezi, mapato ya kila robo mwaka na kila mwaka , pia tumeendelea kufanya utafiti wa pesa mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Alisema baadhi ya utafiti ambao umefanyika ndani ya mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita kuwa ni wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi uliofanyika mwaka 2020/2021 .

"Lengo la utafiti huu ni kupata takwimu za msingi za hali ya soko la ajira ambazo huwezesha kupima na kutathmini utekelezaji wa soko la ajira nchini, pamoja na kufahamu nguvukazi iliyoko, ubora wake, watu wasiokuwa na ajira, ili kuweka mipango ya kimkakati ya kukuza ajira nchini," alifafanua.

Kwa mujibu wa Ruth pia kwa kipindi hicho walifanikiwa kufanya utafiti kuhusu mila, desturi na tamaduni za nchi, ili kufahamu athari zake kwa maendeleo ya watoto wakike na kiume katika kukuza maisha yake ili kuleta usawa wa kijinsia.




Kamanda wa Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa (kushoto), akiwa na wanafunzi wa Shule ya Msingi Olympio jijini Dar es Salaam, wakati wakisikiliza kesi za madereva waliovunja sheria za usalama barabarani kupitia programu ya Mahakama ya Watoto yenye lengo la kutoa elimu ya usalama barabarani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali sasa kutumia fursa za kielimu IST

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameupongeza uongozi wa Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) kwa kukamilisha jengo la masomo, akisema litasaidia kuwaongezea ujuzi wanafunzi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa jengo hilo, alisema alipata fursa pia ya kutembelea madarasa yao na kuona jinsi wanavyojifunza ikiwamo kujiongezea ujuzi.

Alisema shule hiyo wanasoma watoto wa watu wenye uwezo mkubwa wakiwamo mabalozi na wanapata nafasi ya kujifunza mambo mbalimbali, akibainisha kuwa hiyo ni aina ya mabadiliko ambayo Rais Samia Sulihu Hassan ameagiza wayaanzishe.

"Shule hii pia wanatoa nafasi tano kwa Watanzania ambao wanafanya vizuri katika mitihani yao ya taifa ya kidato cha nne, wanaletwa hapa wanasomeshwa bure, na wanapokuwa na safari za kwenda nje ya nchi wanalipiwa na wanaenda na wanafunzi wengine ili wasijione wamebaki nyuma," alisema Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa watafanya mazungumzo na uongozi wa shule hiyo ili kuona namna ya kuongeza nafasi hizo na kwamba ni chache, lakini wanataka kuona zinatawanyika nchi nzima kulingana na jinsi wanafunzi wanavyofanya vizuri katika mtihani wa taifa.

Aidha, alieleza kuwa wataangalia wafanye nini ili waweke Watanzania wengi zaidi kwa sababu wanaopata nafasi hizo wanasoma kidato cha tano na sita na wanapata astashahada inayotambulika kimataifa na itawawezesha kwenda vyuo mbalimbali ikiwamo (Oxford), ambako alisema wako Watanzania ambao wameenda huko kusoma kupitia utaratibu huo.

Pia alisema kuwa Rais Samia aliwapa maagizo ya kupitia mtaala na mfumo wa elimu nchini ili uakisi matakwa yao, mazingira ya wanafunzi na uweze kuwasaidia kuingia katika utandawazi kulingana na dunia inavyokwenda.

Mwenyekiti wa Baraza la Wakurugenzi la IST, Rick Shearn, alisema mradi huo ulitekelezwa kwa muda mrefu, na ana furahi kuona jengo hilo limekamilika akisema kuwa alipojiunga na bodi hiyo kwa mara ya kwanza na kuona eneo la ujenzi wake hakufikiria kama linavyoonekana sasa.

Alisema kutoa huduma zenye viwango vya kimataifa, pamoja na sifa za ubora wa kitaalamu na aina mbalimbali za programu, ni muhimu ili kuhakikisha IST inaendelea kuvutia mashirika tofauti ya elimu kimataifa.

# ‘Jamii isijisahau maambukizi corona’

**Na Jenifer Gilla**

WIKI iliyopita, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakati akitoa tamko la hali ya ugonjwa wa UVIKO-19 kwa miaka miwili tangu kuripotiwa kwake, alisema hadi kufikia Machi 15, mwaka huu, watu 33,789 wamethibitika kupata maambukizi na watu 803 wamepoteza maisha.

Taarifa hiyo iliashiria kupungua kwa mwenendo wa maambukizi ya ugonjwa huo tofauti na miaka miwili iliyopita ambapo idadi ya maambukizi na vifo ilikuwa ikipanda kwa kasi kila mwezi taarifa zinapotolewa.

Alisema kwa kuzingatia hali ya sasa ya maambukizi ya UVIKO-19 nchini na mwenendo wa ugonjwa huo duniani serikali inalegeza masharti kwa wasafiri wanaoingia nchini ambao wamekamilisha dozi ya chanjo ya hiyo kuanzia jana. Licha ya Ummy kusema hivyo, baadhi ya wataalamu wametoa maoni yao, huku wakiweka angalizo.

Mkuu wa kitengo cha magonjwa yanayoambukiza kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Amina Mgunya, alisema kuwa licha ya kuwa tumeudhibiti ugonjwa huu kwa sasa lakini jamii inahitaji kuendelea na tahadhali kama kawaida ili kujikinga.

“Jamii inatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari na kuzifanya kama ni sehemu ya maisha yao, kwa sababu ‘nature’ ya ugonjwa huu, jinsi unavyoambukiza kwa kasi na uwezo wake kujibadilisha umbo na kujiimarisha tukilegeza tu kidogo unaweza kuturudia tena,” alisema.

Alikumbushia tahadhari hizo kuwa ni kunawa mikono mara kwa mara na maji tiririka, kuepuka mikusanyiko isiyo na lazima, na kuepuka kubanana kusikokuwa na lazima, na kuvaa barakoa.

“Sasa hivi utaratibu wa kuweka ndoo za kunawia mikono inabidi uwe sehemu ya maisha yetu na pia mtu unapokoa kuzina mdomo na kiwiko, pia kutembea na vitakasa mikono, tukivifanya hivi tutaudhibiti na kuumaliza kabisa,” alisema.

Dk. Amina pia aliwasisitizia wale ambao hawajapata chanjo waende wakachome, kwa kuwa inasaidia kupambana na maradhi hayo na kupunguza uwezekano wa mtu kuzidiwa pale anapopata maambukizi.

Naye mtafiti wa masuala ya lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe, Wilbert Mgeni, alisema ili kudhibiti ugonjwa huo mpangilio mzuri wa chakula ni jambo la kuzingatia.

“Chakula kina mchango mkubwa katika kwenye kupambana na magonjwa kwa hiyo nashauri watu wazingatie makundi yote ya vyakula katika milo yao ili kupambana na ugonjwa wa COVID-19,” alisema Wilbert.

Alitaja makundi hayo kuwa ni vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi mbichi, nyama na mikunde, matunda, mboga za majani, pamoja na sukari, mafuta na asali.

Naye Msaikolojia Tiba kutoka Hospitali ya Somedics Clinics Center, Saldin Kimangale, alisema ili kuwa na taifa salama katika vita vya ugonjwa huo kila mmoja atekeleze wajibu wake katika kujikinga ili awe salama.

“Suala la kujikinga linapaswa kuanzia kwa mtu mmoja, kwa sababu kila mmoja anakumbuka tulipotoka na wengine walipata maambukizi au kushuhudia ndugu na majirani walivyoteseka na wengine kupoteza maisha,” alisema.




Balozi wa Biko Tanzania, Kajala Masanja (kushoto), akifurahia kumkabidhi Nuru Mikikadi (katikati) Sh. milioni 10 alizoshinda kwenye droo kubwa ya bahati nasibu ya Biko iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. Kulia ni Flamiana Msilu, Meneja Uhusiano wa CRDB Tawi la Premier lililoko Palm Beach, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magonjwa ya saratani tishio kubwa

**Na Christina Mwakangale**

SARATANI ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume zimetajwa kuwa kati ya aina takribani 10 za ugonjwa huo, zinazoongoza kwa ongezeko la wagonjwa na vifo nchini, huku wanawake wakiathiriwa zaidi.

Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Hospitali ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Caroline Swai, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, wakati akiwasilisha mada kuhusu aina tatu kuu za ugonjwa huo, kwenye mafunzo ya kuwajengea uelewa wanahabari.

Mafunzo hayo yalitolewa na Mradi Mtambuka wa Saratani (TCCP) ambao umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Aga Khan Foundation (AKF) unaotekelezwa kwa miaka minne.

Dk. Caroline alisema kila mwaka saratani ya shingo ya kizazi inaongezeka akisema mwaka 2020 maambukizi mapya yalikuwa ni 10,241, huku kila mwaka wanawake 9,772 hugundulika kuwa na ugonjwa huo.

“Wanawake wako katika hatari zaidi, kutokana na kuwa rahisi kupata maambukizi ya virusi vya ‘Human Papilloma Virus (HPV) na umri mkubwa. Pia hata saratani ya matiti wanawake huwa na uwezekano wa kuipata kuliko wanaume, mwaka 2020 kati ya maambukizi 3,992 wanaume waliokuwa asilimia moja,” alisema.

Pia alisema saratani ya tezi dume kwa wanaume inaongoza na kwamba kinga hakuna isipokuwa kwa kubadili mtindo wa maisha, kuacha matumizi ya tumbaku, kupunguza vilevi, kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu na kujenga utaratibu wa mazoezi kila wiki.

“Mwaka 2018 duniani saratani ya tezi dume ni asilimia 7.1 ya saratani zote. Ilisababisha vifo kwa asilimia 38 vya saratani zote pia,” alisema Dk. Caroline.

“Kuchelewa kukoma hedhi, kutowahi kupata mimba, kutowahi kunyonyesha mtoto, umri zaidi ya miaka 50 inaweza kusababisha mwanamke kupata saratani ya shingo ya kizazi au matiti.”

Meneja mradi huo, Dk. Harrison Chuwa, alisema Hospitali ya Aga Khan inatarajia kuanza kutoa huduma ya vipimo na tiba kwa ugonjwa huo, huku ujenzi wa jengo litakalogharimu Dola za kimarekani milioni tano, utaanza mwezi ujao.

Alisema uwapo wa huduma hiyo utaongeza idadi ya hospitali zenye vifaa vya huduma ya saratani nchini ambazo ni Bugando, ORCI, Ifakara ikiongezeka Aga Khan, akisema itakapoanza kuhudumia asilimia 35 watapatiwa huduma bure.

“Asilimia 60 ya wagonjwa wa awali baada ya Aga Khan kukamilisha ujenzi wa jengo la takribani Dola za kimarekani milioni tano, ikianza huduma ya saratani mwakani, watachangia kwa bima ya afya au fedha taslimu,” alisema Dk. Chuwa ambaye ni bingwa wa saratani.

Dk. Chuwa alisema mradi huo unagharimu shilingi bilioni 38 na unashirikisha Wizara ya Afya, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), AKF, Hospitali ya Bugando na ORCI.

# Bidii yatakiwa kukuza sekta vifaa tiba, dawa

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka Watanzania kuweka bidii katika kukuza sekta ya vifaa tiba na dawa kwa kuzingatia ubora ili kushinda mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, wakati akifungua semina ya wadau wa sekta ya dawa na vifaa tiba kuelekea maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika (ARSO).

Dk. Ngenya alisema kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni ‘Jukumu la viwango katika kukuza sekta ya dawa na vifaa tiba Afrika kufikia kujitegemea na ustamilivu katika kupambana na UVIKO-19 na magonjwa mengine ya mlipuko wakati ujao.

Alisema kauli mbiu inawakumbusha kama Taifa kuongeza kasi katika kusimamia sekta ya vifaa tiba na dawa ili kumudu kupambana na maambukizi ya UVIKO-19 pamoja na magonjwa mengine ya mlipuko kwa wakati ujao.

“Tukumbuke ugonjwa wa UVIKO-19 umeshambulia na kusababisha madhara nchini, Afrika na dunia kwa ujumla hivyo maadhimisho haya yanatutaka kuongeza nguvu katika kukuza uchumi wa viwanda hasa kwenye sekta ya dawa na vifaa tiba ili kupunguza gharama nyingi za kuagiza vifaa hivyo na kuzorotesha uchumi wetu,” alisema Dk. Ngenya.

Alisema viwango ni nyaraka ambazo hutayarishwa kwa kuzingatia mfumo wa uwazi, ushirikishaji wa wadau mbalimbali, hivyo vinapokuwa vimekamilishwa na kupitishwa na mamlaka husika, viwango huweka maainisho na misingi muhimu ya kuzingatia katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Alisema matakwa ya viwango yanazingatia kuwezesha kutolewa kwa bidhaa na huduma bora kwa jamii husika, hivyo kulinda afya, usalama na mazingira na hatimaye kuchangia katika uchumi endelevu wa taifa.

Kaimu Mkurugenzi Uandaaji Viwango wa TBS, Yona Afrika, alisema katika kusherehekea siku ya viwango Afrika kwa mwaka 2022, shirika hilo limeandaa shughuli mbalimbali ikiwamo kuandaa warsha zitakazohusisha wadau katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Alisema pia watawashirikisha wakuu wa taasisi ili kuwapa elimu juu ya viwango na mifumo ya kimenejimenti kama ISO 9001, ISO 14001 na nyinginezo ili kuwezesha taasisi zao kutoa huduma zinazokidhi viwango vya kimataifa.

“Pia tumeandaa semina za kutoa elimu kwa maofisa wa Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu masuala ya viwango,” alisema.

Mshindi wa kwanza kwa ngazi ya bara atapata fursa ya kushiriki mkutano mkuu wa ARSO utakaofanyika nchini Cameroon Juni mwaka huu.




Ukurasa 13

Inazalisha mkaa wa maboksi, vifuu, majani ya miti, nyasi, vumbi mbao

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 22, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Waingia mtaani kuelimisha vita vya ngono 'mpaka kieleweke'**

ELIMU

NA JOSEPH MWENDAPOLE

# Chuo Kikuu Ardhi, wasomi wenzao wajifungia kujadili utafiti miaka 5

- Unachambua hatima ya mazingira nchini
- Waziri Mkenda: Msiwabugudhi maprofesa
- Awaasa: Kazi zao mbona mtasahau bajeti!



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, akiangalia bidhaa zilizotengenezwa kwa mabaki ya mazao kutokana na utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu Ardhi (ARU), alipokwenda kufungua mkutano wa kimataifa kuhusu ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

INAPOTAJWA taasisi yoyote ya elimu ya juu, ina wajibu unaoangukia mambo matatu makuu; kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri nasaha.

Hicho ndicho kitarajie kinapatikana, iwe katika chuo kikuu au kingine kinachotoa elimu, ngazi ya digirii. Hivyo, hata pale inapojadiliwa ubora wa taaluma katika maeneo hayo, moja kwa moja inapaswa kuangukia katika utafiti na huduma bora za ushauri.

Mwanasiasa mwanadamizi nchini, James Mbatia, ambaye naye amebahatika maishani kukanyaga ardhi ya elimu ya juu, huwa anapenda kusisitiza kaolin 'hoja kwa vielelezo', akimaanisha kila hoja iwe na utetezi wenye wa kitafiti ua marejeo fulani. Ujumbe mkubwa anahitaji usomi katika hoja zake.

Ni aina ya usemi ambao umekuwa ukihimizwa na aliyekuwa Rais wa China, Mao Tse Tung, hata kugeuka kuwa tamathali ya kudumu inayopatikana nchini China.

Pia kuna wakati aliyewahi kuwa Ofisa Taaluma Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Prof. Penina Mlama, katika hafla ya kutimiza miaka 20 ya Kitivo cha Sanaa cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuhusiana na viwango vyao vya utafiti.

Kwa mujibu wa mwanazuoni huyo ambaye alikuwa mwalikwa, aliweka angalizo kwamba suala la kushuka viwango vya utafiti kuna uhusiano wa moja kwa moja na kuathirika taaluma.

**KUTOKA KWA WATAFITI**

Ndani ya mustakabali huo, hivi karibuni Chuo Kikuu Ardhi (ARU), kilifanya kongamano la kimataifa la siku mbili jijini Dar es Salaam kujadili kuhusu utafiti uliofanywa na chuo hicho kuhusu masuala ya ardhi, mazingira ya mabadiliko ya tabianchi kati ya mwaka 2017 na 2022.

Hiyo ni za lao utafiti wa namna tofauti unaofanywa na chuo hicho, kuibua matokeo yenye manufaa kwa umma na hatua hiyo mpya, imekuwa ya wasomi hao kukusanyika na kujadili maudhui ya kazi hiyo chini ya Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA).

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambaye pia msomi mwenzao wa wazuoni hao wa ardhi, Prof. Adolph Mkenda, ndiye alikuwa mgeni rasmi kwenye kongamano hilo la siku mbili akiwa na hoja kuu ya anayowahimiza nayo wasomi wenzake katika aina ya taasisi alikotokea, wanapaswa wajitahidi kujitegemea.

Anasema, vyuo vikuu badala ya kusubiri mafungu kutoka serikalini vinapaswa kuwa na mbinu za kujenga uhusiano na vyuo na taasisi nyinginezo duniani kupata miradi yenye uwezo wa kuwaingizia kipato na kuacha utegemezi mkubwa serikalini.

Anawasifu Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Evaristo Liwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Balozi Salome Sijaona, wamejitahidi kujenga uhusiano mzuri na vyuo, pia taasisi nyinginezo duniani na sasa wananufaika na uhusiano huo kiuchumi.

"Mimi ningependa kuona juhudi zinazofanyika hapa ARU zinafanywa na Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, naambiwa wanafanya juhudi hizi, lakini ningependa kuona wanaongeza bidiii ili Mzumbe na wengineo..." anasisitiza.

INAENDELEA UK.12

# Chuo Kikuu Ardhi, wasomi wenzao wajifungia kujadili utafiti miaka 5



Daraja la Mto Mpiji lililokatika na kusababisha wakazi wa Bagamoyo kushindwa kufanya shughuli zao, ikiwamo kukwama mawasiliano na jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.11**

Hapo msomi huyo ana anagalizo la kuwatunza wasomi wenzake wakiwamo maprofesa wenye uwezo mkubwa wa kuandaa maandiko hayo muhimu, hata yakawashawishi wafadhili kutoa hela kwa vyuo vyao na kamwe si kusakamwa na mamlaka za juu yao.

Profesa Mkenda akitumia kigezo 'hoja kwa vielelezo' anatoa mfano kuna wakati ameshuhudia mradi mmojawap ambao ufadhili wake umewezesha unasomesha Watanzania na kununua makaratasi na mashine za kurudufia.

"Nadhani si sahihi kutoza kodi kwenye vitu vya msaada kwa sababu wenyewe wanaweza kuondoa na hata kupeleka kwenye vyuo vingine kama Makerere (Uganda) na kwingineko ambako hawatozi kodi na vikwazo vingine tuviondoe ili kuvutia miradi mingi ya msaada kwenye vyuo," anafafanua.

Anasema uzoefu uko wazi kwamba wasomi ngazi ya maprofesa na viwango vinavyofanana navyo duniani, wamekuwa na manufaa kwa taasisis zao kwa kuandaa maandiko yenyue miradi muhimu kwa taasisi zao, kwani imewavutia wafadhili.

Profesa Mkenda akiwa na ujumbe mpana unaofika kwa vyuo vikuu vingi nchini, vya umma na binafsi, anadema vhuo hivyo vimekuwa vikipata fedha na kuwa mkombozi mkubwa kwa maendeleo yao na hata kuondokana na utegemezi.

> Unaweza kuwaza kwa mfano Jiji la Dar es Salaam litakuwaje kama hakuna daraja la selander, Jangwani au barabara ya Kigogo au mji wa Dodoma bila chanzo cha maji cha Makutopora.



Eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, ambako huwa kunaathirika na mafuriko. Vyote ni sehemu ya athari za mazingira.

"Vyuo vyote duniani havitegemei fedha za serikali tu, bali kupitia miradi inayoandikwa na maprofesa wao, wanafanya hivyo Afrika Kusini, Misri, Marekani na Sweden, hivyo hakuna sababu ya Tanzania kushindwa kuandika miradi, maprofesa wazuri wapo wapeni nafasi na muwawezeshe," anasema.

Prof. Mkenda, katika halfa hiyo hoja na uwasilishi wake uliegemea zaidi taaluma yake zaidi ya darasani, kuliko wajibu mkuu wa kiutawala alio nao sasa, ingawa bado una joho 'wizara elimu'.

Anawasisitizia wanazuoni waandamizi wakiongozwa na maprofesa wawezeshwe, kisha kuwawekea vikwazo na hata wanapotaka kusafiri nje ya nchi waruhusiwe.

**ARDHI WAFUNGUKA**

Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Gabriel Kassenga, anasema mkutano umewashirikisha wataalamu wa masuala ya ardhi mabadiliko ya tabianchi na mazingira, ili kubadilishana mawazo ya kisomi kuhusu matokeo ya utafiti huo yatakavyoboresha sera za ardhi na mabadiliko ya tabia nchi.

Anasema chuo hicho kimewatumia wasomi wake kufanya utafiti aina nyingi na kuja na bidhaa za kosomi, ambazo hata zitafanyiwa kasoro kibiashara zaidi zitaweza kuingizia mapato mengi na kuvitaka vyuo vingine kuiga ubunifu kama huo.

"Nakipongeza pia chuo hiki kwa kujenga uhusiano na Shirika la SIDA- Sweden hali ambayo imewezesha Watanzania watafiti kupata ufadhili wa kufanya tafiti na wengine kwenda kusoma nchini humo," anasema.

Kwenye mada kuhusu mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Prof. Kombe Wilbard, anasema mabadiliko ya tabianchi kuna wakati yamesababisha majanga kwa watu na mali zao kupotea, hasa penye makazi yasiyo sahihi holela.

Anasema miji mikubwa imekuwa ikiathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi, kutokana na idadi kubwa ya watu na kukosa miundombinu bora, hasa nyakati za mvua kubwa, hata kushuhudiwa mafuriko.

Prof. Wilbard, anasema mara nyingi wananchi kutoka familia duni zinazoishi kwenye makazi yasiyo na mpangilio, wamekuwa wakikumbwa na majanga wakati wa mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu wamekuwa hawajaiandaa na kukabiliana na mazingira hayo.

Anasema miundombinu kama ya barabara, madaraja, hospitali, nishati na ya usambazaji wa maji ni muhimu kwa ustawi wa jamii kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Dodoma.

"Unaweza kuwaza kwa mfano Jiji la Dar es Salaam litakuwaje kama hakuna daraja la selander, Jangwani au barabara ya Kigogo au mji wa Dodoma bila chanzo cha maji cha Makutopora," anasema.

Aidha, profesa huyo anasema kuna umuhimu wa kuwa na takwimu na taarifa sahihi zitakazosaidia kuwapo kwa uelewa wa pamoja kwa wananchi kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi.

"Tukielewa vizuri kuhusu athari za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi zitasaidia jamii zetu na watunga sera kuweka mipango mizuri ambayo itasaidia kukabiliana na majanga," anahitimisha msomo huyo.

TEKNOLOJIA
NA SABATO
KASIKA

MASHINE AINA YAKE;

# Inazalisha mkaa wa maboksi, vifuu, majani ya miti, nyasi, vumbi mbao

MATUMIZI ya nishati mbadala yanahimizwa kila mara kwa kunusuru mazingira kutokana na ukweli kwamba ukataji miti kwa ajili ya mkaa, umeshamiri katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia ukataji huo wa miti kwa ajili ya mkaa unaotumika kwenye shughuli mbalimbali zikiwamo kupikia, unatajwa kuwa ni fursa kubwa ya kipato kwa baadhi ya watu hasa vijana ambao hutegemea biashara hiyo kwa ustawi wao.

Ni hali inayowafanya wadau wa mabadiliko ya tabianchi kushauri kuwapo nishati mbadala, haraka na katika mazingira endelevu.

Zimekuwapo jitihada mbalimbali za kusaidia kunusuru mazingira, ikiwamo kutengeneza mashine zinazozalisha nishati mbadala zisizotumia miti na kuacha mazingira salama, Ili kutunza mazingira kwa kutumia nishati mbadala.

Baadhi ya watu, vikundi, taasisi na vituo kadhaa, vimekuwa vikizalisha nishati mbadala kwa kutumia mashine hizo ambazo ni maalumu kwa utunzaji huo wa mazingira.



Akikusanya mkaa kwa ajili ya kuweka katika mashine ili uchakatwe. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

### WAHUSIKA WALIOIBUKA

Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni jijini Dar es Salaam, katika orodha ya waliobuni mashine ya aina hiyo inayozalisha mkaa kwa kutumia maboksi, vifuu vya nazi, majani ya miti, nyasi na vumbi la mbao.

Mashine hiyo imetolewa na Shirika la Utafiti na Tiba Barani Afrika (AMREF) Januari mwaka huu na kwamba hivi karibuni limewapa pikipiki aina ya Toyo itakayotumika kusomba malighafi za kutengenezea mkaa huo.

Mwendesha mashine hiyo, Juma Rashid, anasema kazi inaanza kwa kukusanya maboksi, vifuu vya nazi, majani ya miti, nyasi na hata vumbi la mbao analoweka vyote kwa pamoja katika tanuru la moto.

"Baada ya kuungua, ninatoa na kuweka maji kidogo kisha ninachanganya na uji wa mhogo au uji wa udongo wa mfinyanzi na kuweka katika mashine kwa ajili ya kuchakata na kupata chenga na vipande vya mkaa," anaelekeza mtaalamu Rashid.

Rashid anafafanua kuwa, sababu ya kuweka uji wa muhogo au uji wa udongo wa mfinyanzi ni kutaka mchanganyiko huo, anataka upate ili iwe rahisi kuufinyanga kwa saizi

> Ninyi Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni au Sauti ya Jamii Kipunguni, mna vitu vingi ambavyo watu wanaweza kuja kujifunza kwenu, nitahamasisha wengine waje hapa kupata maarifa.



Juma Rashid akipanga vipande vya mkaa ambao tayari umetengenezwa.

ya vipande wa mkaa wanavyotaka.

Mwendesha mashine hiyo, anafafanua kuwa wakishafinyanga kupata vipande vya mkaa vya saizi wanayoitaka, wanavinakausha juani kwa muda wa siku tatu hadi nne vinakuwa tayari kutumika.

"Hatujaanza kufanya uzalishaji wa mkaa kwa ajili ya biashara, bali tumefanya majaribio, wakati tukisubiri uzalishaji rasmi baada mashine kuzinduliwa na wafadhili wao AMREF miezi michache ijayo," anasema.

Rashid anaeleza kwamba, yeye ni kati ya wanachama wanaounda kituo hicho waliopata mafunzo ya ujasiriamali katika Semina za Jinsia na Maendeleo zinazofanywa kila Jumatano na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Anaeleza kuwa shirika la AMREF waliona juhudi za kituo hicho na wakawapa mashine hiyo, kwa ajili ya kuendeleza ujasiriamali wao wainuke kiuchumi, kwa kuzalisha mkaa kwa njia hiyo ambayo unachangia kulinda na kutunza mazingira.

"Tayari viongozi wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) walishatambelea kituo chetu na kuona mashine hii inayozalisha nishati mbadala ya kutukabidhi cheti kinachoonyesha kuitambua," anasema.

### DK. GWAJIMA AKUNWA

Katika ziara yake kituoni hapo hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, anakipongeza kituo hicho kuwa mfano wa kuigwa kwa jinsi kinavyoendesha shughuli zake, ikiwamo kuzalisha mkaa mbadala kwa ajili ya kutunza mazingira.

"Hongereni kwa kupata mashine, kwani teknolojia kama hii ndiyo inayohimizwa ili kulinda mazingira yetu, ninatamani ziwe nyingi ili ikiwezekana, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa uishe," anasema Dk. Gwajima.

Waziri huyo anaeleza imani yake kuwa juhudi zinazofanywa na uongozi wa kituo hicho, ndizo zilizozaa matunda ya upatikanaji wa mshine hiyo na akashauri vikundi, vituo na taasisi nyingine kuiga mfano kwa kituo hicho.

"Ninyi Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni au Sauti ya Jamii Kipunguni, mna vitu vingi ambavyo watu wanaweza kuja kujifunza kwenu, nitahamasisha wengine waje hapa kupata maarifa," anasema.

Waziri Dk. Gwajima anaongeza:" Mna mashine inayotumia teknolojia ya kisasa kutengeneza mkaa mbadala, mna shule ya ushonaji na saluni, mnafundisha bure manusura wa vitendo vya ukatili, hili ni jambo jema."

Mwenyekiti wa kituo hicho, Fatma Talib, anasema huwa wanatoa mafunzo ya ufundi cherehani na saluni tangu mwaka 2016, na kwamba tangu wakati huo, wanafunzi 360 walishahitimu ufundi cherehani.

"Pia wapo mabinti 15 ambao walishahitimu mafunzo ya saluni, wote hao wakiwa ni 'manusra' wa vitendo vya ukatili hasa ukeketaji, katika Kata hii ya Kipunguni," anasema Fatma.

Fatma anawataja wadau wao wakubwa kuwa ni TGNP, kwamba ndiyo 'waliowapika'kupitia semina za kila Jumatano na kuwapa mafunzo ya sheria ambao wamekuwa ni wasaidizi wa kisheria katika jamii, kwa kushirikiana na orodha ya wadau wengine na mashirika yasiyo ya kiserikali.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Waingia mtaani kuelimisha vita vya ngono 'mpaka kieleweke'

## • Mdau Gema: Nimefurahi vibanda kuvunjwa




Mkurugenzi wa Women Tabata TAPO, Stella Mbaga akizungumza kwenye kongamano la wanawake lililoshirikisha wadau kadhaa ikiwamo jeshi la polisi, viongozi wa mitaa, wanaharakati na wadau mbalimbali. Kulia Mkurugenzi wa Women Fund, Rose Marandu na Mwanaharakati ngazi ya jamii, Gema Akilimali (kushoto). **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

MWEZI Machi unatajwa kuwa ni wao wanawake waliojipangia duniani, hata kwa kubeba siku maalumu kwa ajili yao ambayo huadhimishwa kila mwaka, tarehe 8.

Wanawake hao katika maadhimisho tofauti wanaelezea ujumbe wao tofauti kwenye jamii vikiwamo vikwazo na matukio ya ukatili wa kijinsia pamoja na juhudi za serikali, wadau na wanaharakati kuendelea kutoa elimu.

Shughuli zinazofanywa na wanawake hawa ikiwamo za kiuchumi na kutoa mchango mkubwa kwenye malezi ngazi ya familia, jamii na taifa kunalifanya kundi hili kuendelea kutambulika, hata takwimu zikitetea.

Mkurugenzi wa Asasi ya Women Tabata TAPO, Stella Mbaga, katika kuadhimisha siku hiyo mwezi huu anasema sasa shirika hilo linaanza kufanya kampeni ya kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia na kutetea haki za wanawake na watoto kwenye maeneo ya mitaa, shule kwa kushirikiana na viongozi wa Wilaya ya Ilala.

Stella amebainisha hayo kwenye kongamano la wanawake lililoshirikisha wadau kadhaa, likiwamo Jeshi la Polisi, viongozi wa mitaa, wanaharakati na wadau, waiwamo Women Fund.

"Kongamano hili limewaleta pamoja wadau ili kujadili na kila mmoja kuelezea kilichoko katika jamii, itasaidia sauti hizi kupazwa kwenye vyombo vya habari, hatua kuchukuliwa pamoja na jamii kubadilika, kwa sababu bado matukio ya ukatili ni mengi kwenye mitaa yetu tunamoishi," anasema Stella.

### WADAU WAFUNGUKA

Mwanaharakati ngazi ya jamii, Gema Akilimali anasema bado kuna vikwazo katika jamii ikiwamo rushwa ya ngono hususan maeneo ya shughuli za kiuchumi kama vile sokoni ni kikwazo kufikia maendeleo.

"Rushwa ya ngono imetamalaki. Mfano maeneo ya sokoni kinamama ili apate meza afanye biashara mlolongo mrefu. Tatizo la rushwa ni kwa sababu ni tukio la watu wawili anayefanyiwa akikaa kimya kuupata ushahidi ni changamoto," anasema Gema.

Gema anasema mara kadhaa amekuwa kishiriki kutoa elimu kuhusu kupinga matukio ya ukatili hivyo hata mtaani anakoishi jamii humshirikisha masuala kadhaa.

"Vibanda vya biashara vilivyotolewa barabarani tunashukuru, mimi kama mwanaharakati nasema hivi kwa sababu eneo hilo lilikuwa sehemu ya ukatili kwa mabinti. Vibanda vilitumika kwa ajili ya ngono kwa mabinti ilikuwa kama 'butter trade' wanapewa vichips kidogo kisha kinachoendelea huko ndani mzizi, mlezi hutapenda kusikia.

> "Rushwa ya ngono ipo. Baadhi ya ufaulu kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mabinti tulibaini kipimo ni rushwa ya ngono. Ukipata uongozi kwa njia ya rushwa ya ngono hautaheshimika.

"Niliwahi kuitwa siku moja hapa hapa mtaa mojawapo Tabata nikaambiwa nikashuhudie ninachokisema hapa. Nilikuta binti yupo na mwenzie anamwambia mwenzie tangulia wewe, ni kama maigizo lakini ndio hali halisi. Nilichokiona nilikifikisha TAMWA na walifanya uchunguzi wao," anasema Gema.

Mkurugenzi wa Asasi ya Women Fund, Rose Marandu, akiwa mgeni rasmi kwenye kongamano hilo anasema rushwa ya ngono inamkandamiza mwanamke na kumwondolea utu wake na kushindwa kujiamini.

"Rushwa ya ngono inadhalilisha na inaua. Wengine wanapata msongo wa mawazo, baadhi taarifa zao husambaa mtandaoni wakiwa wamerekodiwa video baada ya kuahidiwa kupata fursa fulani anakubali kurekodiwa.

"Fikiria taarifa iwe mtandaoni hata picha akiwa utupu, inadhalilisha na wengine hujiua kila siku tunasikia matukio haya," anatamka Rose- Mkurugenzi wa Women.

Anabainisha, kutokana na hilo shirika limeshaanza na kampeni ya 'safiri salama' ambayo inalenga usafiri salama kwa kushirikiana na madereva wa bodaboda, bajaji na daladala, ili kila binti hasa mwanafuzi anayetumia usafiri afike salama salimini aendako.

Rose anaeleza kampeni hiyo, pia inakwenda sambamba na ushirikiano kati yao na vyombo vya kisheria kuhakikisha sheria zilizoko zinafanya kazi.

"Rushwa ya ngono ipo. Baadhi ya ufaulu kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mabinti tulibaini kipimo ni rushwa ya ngono. Ukipata uongozi kwa njia ya rushwa ya ngono hautaheshimika.

"Tujiamini kwa kupitia ushindani ulio wa haki, tujiamini kushika nafasi za uongozi na kuwa na uchumi mkubwa bila kutegemea kusimamiwa na mtu fulani," anasema Rose.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Tabata, Fatuma Katurwa, akitoa elimu kwenye kongamano hilo, anasema familia na jamii iwajengee watoto wa kike misingi imara ili kuwa viongozi bora.

"Baba yangu katusomesha mabinti tupo saba katika familia yetu. Lakini, jamii ilimshangaa mzazi wangu kwa kutusomesha wanawake, wakisema hao si wa kwenda kuolewa tu, utasomeshaje wasichana..." anasema Fatuma.

### DAWATI LA JINSIA

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto (Wilaya) Buguruni-Tabata, Inspekkta Fransiska Nunduma, anasema takwimu za matukio ya ukatili kijinsia hutofautiana msimu na msimu, kupanda au kushuka.

Anasema kipindi ambacho shule zinafunguliwa matukio ya ukatili kijinsia huongezeka zaidi, ikilinganishwa na msimu ambao shule huwa zimefungwa.

"Sababu kuu ya unyanyasaji kijinsia ni ndoa, mahusiano. Utakuta wazazi wanapotengana uutakuta watoto ndio wanaathiriwa sababu malezi yanakuwa si ya pamoja. Kinachotakiwa ni jamii kuzingatia malezi, shule na makuzi yao," anasema Insp. Fransiska.





## Jeshi la Polisi lapewa mbinu kukabiliana na uhalifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonaz, ameli-taka Jeshi la Polisi, kujifunza kila siku namna ya kukabiliana na uhalifu wa kimtandao ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia.

Pia ameiagiza jamii ipewe elimu ya kutambua makosa ya kimtandao na namna ya kuchukua tahadhari ili kujiepusha kushiriki kwenye makosa hayo.

Dk. Yonaz alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo kwa viongozi mbalimbali wa jeshi hilo kuhusu makosa ya kimtandao.

Alisema dunia inabadilika, kuna uhalifu wa kimtandao ambao unapaswa polisi kufuatilia kwa makini na kukabiliana nao.

"Mfano mgogoro wa Ukraine na Urusi najua nyie kama askari mnafuatilia kwa makini kabisa kinachoendelea najua mnatambua pamoja na kupigana vita physical, lakini kuna vita ya kidijitali," alisema.

Alisema mafunzo hayo yanawapatia njia ya wapi waelekee hasa kwenye masuala ya usalama wa kimtandao.

"Ni muhimu tukitoka hapa ukumbuke una wajibu wa kujifunza kila siku, mafunzo haya ni muhimu sana yameelekezwa kutoonesha njia ya nini tunatakiwa kufanya ili kuhakikisha usalama wa raia unakuwa timamu," alisema.

Kadhalika, alisema wizara hiyo ina wajibu wa kuhakikisha usalama katika mtandao unazingatiwa vizuri.

"Mafunzo haya ni endelevu kwasababu teknolojia zinabadilika, teknolojia za jana na za leo ni tofauti na zinabadilika kwa maana kwamba speed ya processing inaongezeka mawasiliano yanazidi kuwa haraka, pia namna taarifa zinavyotengenezwa na kuhifadhiwa," alisema.

Alisema wizara itahakikisha inajenga uwezo wa vifaa, utambuzi, utaalamu ili kufanikiwa kukabiliana na uhalifu wa kimtandao.

"Mafunzo haya ni muhimu kutokana na aina ya maisha tunayoendelea nayo, lakini maendeleo ya sayansi na teknolojia, hivyo ni muhimu sisi tulioko hapa tunakuwa walimu kwenye maofisi yetu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camilius Wambura, alisema mafunzo hayo yanahusisha washiriki 100 ambao wote ni kutoka kwenye jeshi hilo nchini.

Alisema malengo ni kila askari kuwa na elimu kuhusu makosa ya kimtandao kutokana na sasa uhalifu wote umehamia kwenye eneo hilo.

"Ni ukweli usiopingika kwamba teknolojia inabadilika kila kukicha hivyo huhitaji mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji wetu ili kuendana na kasi ya mabadiliko hayo ili kufikia lengo la kupambana na uhalifu huo," alisema.

# Uongozi Mto Wami-Ruvu watakiwa ubunifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UONGOZI wa Bonde la Mto Wami-Ruvu umetakiwa kuandaa mpango wa ubunifu wa kuanza maandalizi ya upandaji wa miti katika eneo la ekari 309 kwenye chanzo cha maji Mzakwe mkoani Dodoma ili kulinda eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki kwenye ziara ya kukagua na kujionea upandaji miti katika Bonde la Mzakwe ambalo ni chanzo cha maji yanayosambazwa katika Jiji la Dodoma.

Mtaka aliongozana na wataalamu wabobevu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI), Taasisi ya Watafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Dodoma na Bonde la Wami-Ruvu na walifikia mwafaka na kutafuta mwarobaini wa kunusuru miti iliyopandwa na kupanda mingine itakayostahimili ardhi ya bonde hilo.

Alisema Mamlaka ya Bonde la Mto Wami-Ruvu ndiyo msimamizi wa eneo hilo na kushauri wafanye maandalizi ya mpango huo ili uwe na matokeo chanya.

"Mpango huo utekelezaji wake unatakiwa kuwa msimu wa mwaka 2022/23, uoneshe hatua za kuandaa eneo, uchimbaji wa mashimo na uandaaji miche na kunapofika kipindi cha masika, miti hiyo ipandwe ili kukijanisha bonde hili Mzakwe," alisema Mtaka.

Mkuu huyo alisema kuwa lazima utafutwe mwarobaini kuhakikisha miti inayopandwa kwenye eneo hilo inadumu na kustawi bila kuharibu chanzo muhimu cha maji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwataka viongozi wa bonde hilo kusimamia azma hiyo ya kukijanisha bonde kufanya maandalizi ya kupanda miti ya aina mbalimbali inayostawi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Bonde hilo, Mhandisi Elibariki Mmassy alisema, wapo tayari kusimamia na kuunganisha utaalamu kuhakikisha mpango wa kupanda miti katika bonde hilo ili ufanikiwe.

Mhandisi Mmassy alisema kuwa watahakikisha wanaweka alama na kuchonga barabara kuzunguka eneo lenye ukubwa wa kilometa 460.

Mbobevu katika masuala ya misitu kutoka Ndaki ya Misitu Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA), Prof. Salim Malionde, alisema wapo tayari kutoa ushauri na utaalamu kwa kamati ya usimamizi wa mradi huo ili kuhakikisha miti itakayopandwa inastawi.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI), Dk. Revocatus Mushumbusi, alisema watatoa ushauri na kutambua miti inayofaa kupandwa katika aina ya udongo ulioko hapo na kushiriki kikamilifu katika kutoa mchango wa kiushauri na kuhakikisha utunzaji wa miti.

Dk. Mushumbusi alisema miti jamii ya Acacia imekuwa katika eneo hilo kwa muda na hivyo wamekubaliana kuipanda kwenye eneo hilo.

Mkuu wa Kikosi cha JKT Makurupora, Luteni Kanali Festo Mbanga, alisema watahakikisha mifugo haingii katika eneo hilo kwa muda na wapo tayari kutumia vijana hao kuchimba mashimo hayo watakaposhauriana na uongozi wa bonde.



Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, akizungumza na wenyeviti wa serikali za mitaa ya Halmashauri ya Jiji kwenye semina ya elimu elekeze kwa ajili ya uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi katika mitaa yao, iliyofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wafanyabiashara waonywa kusababisha migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, Steven Maufi, amewataka viongozi wa umoja wa wafanyabiashara wa masoko kutokuwa chanzo cha kuhamasisha migogoro isiyo na tija na kuisababishia halmashauri kushindwa kupata mapato.

Maufi aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa soko kuu la Majengo jijini hapo ambao wanaotarajiwa kufanya uchaguzi wa viongozi mwishoni mwa mwezi Machi, mwaka huu.

Alisema viongozi wanaopewa dhamana ya kuongoza wanatakiwa kuwa mfano bora wa kuhakikisha wanashirikiana katika kutatua migogoro na sio kuhamasisha.

"Niwaombe viongozi ambao mtakaochaguliwa kwenye muhula wa kipindi mtakachokaa madarakani cha miaka mitatu mhakikishe mnatatua migogoro na kuhimiza ukusanyaji na mapato bila kusahau kufanya mikutano yenu kwa mujibu wa katiba yenu," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara ndani ya masoko wanaogombea nafasi mbalimbali kujinadi kwa sera zitakazowanufaisha kibiashara ili kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

"Ninawaomba wagombea wote wanaogombea nafasi mbalimbali, mhakikishe mnatumia sera za kistaarabu na huku mkitumia lugha iliyo staha," alisema.

Uchaguzi wa soko kuu la majengo unatarajiwa kufanyika Machi 30, mwaka huu na nafasi zinazogombewa ni pamoja na Mwenyekiti wa soko na msaidizi wake, katibu na msaidizi na mtunza hazina na wajumbe wa kamati kuu.



# MUST yashauriwa kubuni mbinu udahili

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imeagiza uongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kubuni mbinu za kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kwenye fani za sayansi.

Kamati hiyo ilitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki ilipofanya ziara ya kukagua mradi wa upanuzi wa chuo hicho hasa kwenye miundombinu ya mabweni, karakana, maabara na maktaba na ilibaini kuwa udahili wa wanafunzi wa kike katika chuo hicho ni chini ya asilimia 30.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, alisema idadi ya watoto wa kike wanaosoma kwenye chuo hicho ni ndogo hali inayoashiria kuwa hamasa ni ndogo.

Aliwataka viongozi wa chuo hicho kuongeza hamasa kwenye shule mbalimbali ili kupata idadi ya wanafunzi wa jinsi hiyo ambayo itakuwa inawiana na wa kiume.

"Tunasisitiza hamasa iongezwe kwa watoto wa kike kujiunga na chuo hiki, idadi ya kundi hilo hairidhishi hata kidogo japokuwa Naibu Waziri ametoa maelezo, lakini tunawataka mwongeze hamasa na ubunifu," alisema Nyongo.

Aliagiza hata mabweni yanayojengwa kwenye chuo hicho watoto wa kike wapewe kipaumbele kukaa humo ili wawe kwenye mazingira rafiki zaidi.

Akitoa taarifa ya udahili wa wanafunzi katika chuo hicho, Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST, Prof. Aloyce Mvuma, alisema idadi ya wanafunzi wa kike wanaodahiliwa chuoni hapo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema kwa mwaka huu idadi ya wasichana wanaodahiliwa chuoni hapo kwa miaka mitatu mfululizo 2019/2020, wanafunzi wa kike walikuwa asilimia 19 mwaka 2020/2021 walikuwa asilimia 22 na kwa sasa wameongezeka na kufikia asilimia 23.4.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikitumia mbinu mbalimbali za kuhamasisha watoto wa kike kusoma masomo ya Sayansi ikiwa ni pamoja na kutembelea shule za Sekondari kwa lengo la kutoa elimu na hamasa kwa kundi hilo.

Pia katika chuo hicho wanawake wamepewa nafasi ya kuongoza vitengo mbalimbali nyeti kama mbinu mojawapo ya kuhamasisha kundi hilo.

"Lakini kwenye ngazi ya cheti tumefikia hatua nzuri ambapo inakaribia kufikia asilimia 50 kwa 50 kati ya wanafunzi wa kike na wa kiume, tatizo ni kwamba kadri inapopanda ngazi ya juu ndio idadi inazidi kupungua na kuna mipango yetu ya kuongeza udahili lakini ipo pia ya kiserikali," alisema Prof. Mvuma.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema serikali ina mpango wa kujenga shule moja ya sekondari ya wasichana katika kila mkoa nchini kwa lengo la kuongeza idadi ya wasichana wanaosoma masomo ya sayansi. Alisema baada ya shule hizo kuanza kuna matumaini kuwa idadi ya wasichana wanaojiunga na fani za sayansi itaongezeka na kwamba kuna uwezekano miaka michache ijayo kutakuwa na uwiano sawa.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo (katikati), pamoja wajumbe wa kamati hiyo wakisalimiana na watumishi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) mwishoni mwa wiki walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya upanuzi wa chuo hicho, kushoto ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbarali yapania kukusanya billioni 38/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya Mbarali mkoani Mbeya, imedhamiria kukusanya Sh. bilioni 38 .7 kutoka vyanzo mbalimbali kwa lengo la kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbarali, Twalib Lubandamo, alisema licha ya kuweka makisio ya Sh. bilioni 38.7 bado wameweka baki ya mwaka 2020/2021 Sh. milioni 747 na kufanya jumla ya mapato yote kuwa Sh. bilioni 39.4.

Alifafanua kuwa kwa Septemba 2021 halmashauri ilikusanya Shilingi bilioni tatu kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya halmashauri ikiwa ni sawa na asilimia 106 ya lengo la mwezi la Shilingi bilioni tatu na kufikisha jumla ya mapato ya Shilingi bilioni tisa yaliyokusanywa hadi sasa ikiwa ni asilimia 24 ya lengo la mwaka.

"Kwa mapato ya ndani, halmashauri ilikusanya Sh. milioni 445 kwa mwezi Septemba 2021 ikiwa ni asilimia 108 ya lengo la mwezi la Sh. milioni 411 na kufikisha jumla ya mapato ya Shilingi bilioni moja yaliyokusanywa hadi sasa ikiwa ni asilimia 34 ya lengo la mwaka bilioni nne," alisema Lubandamo.

Kwa kuzingatia bajeti hiyo, halmashauri imepanga kuboresha stendi ya mabasi ya Rujewa ili kuzuia maji kutuama kwa kuzingatia ukarabati wa choo.

Alisema miongoni mwa miradi itayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya pamoja na miundombinu ya barabara na madaraja.

Kwa upande wake, Diwani Bahati Salum, alisema halmashauri imetenga Sh. milioni 10 kwa ajili ya maboresho ya ukarabati wa Zahanati ya Imalilo Songwe ili kusaidia upatikanaji wa maji, ujenzi wa vyoo pamoja na upanuzi wa chumba cha kujifungulia.

# Madalali, mawakala kurasimishwa walipe kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amewataka wadau wa biashara nchini kuandaa mwongozo utakaowezesha madalali na mawakala kurasimishwa ili walipe kodi itakayosaidia kazi hiyo kuchangia pato la taifa.

Alisema serikali inapoteza fedha nyingi kwenye sekta hizo kwa sababu hakuna mfumo rasmi wa kuwatoza kodi licha ya watu hao kukusanya fedha nyingi kupitia shughuli wanazozifanya.

Mgumba aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifunga mafunzo ya Sheria na Leseni kwa maofisa biashara wa halmashauri kutoka mikoa mitatu ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo yaliandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Mafunzo hayo yaliwashirikisha maofisa biashara zaidi ya 50 kutoka katika halmashauri za mikoa ya Mbeya, Songwe na Rukwa na kufanyikia jijini Mbeya kwa muda wa wiki moja.

Mgumba alisema ni wakati wa wataalamu hao wa biashara kuwa wabunifu kwa kuwa na jicho la kuibua vyanzo vingine vipya vya mapato ili kuiongezea serikali mapato yatakayoisaidia kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Niwaombe BRELA na maofisa biashara mkakae muone ni kwa namna gani mnaweza kuwarasimisha madalali kwa sababu katika eneo hili serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi sana, mwenye nyumba hamfahamu mpangaji wake, madalali wamekuwa watu wa katikati na wanapata fedha nzuri sasa," alisema Mgumba.

Alisema endapo kundi hilo litatambuliwa na kuwekewa miongozo na wakapatiwa leseni, serikali itapata fedha na wao wataendelea kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Hata hivyo, mkuu huyo wa mkoa aliwataka maofisa biashara kuwa daraja kati ya wafanyabiashara na serikali na kutokuwa kikwazo cha biashara za watu kukua na wala wawekezaji kuogopa kuwekeza kwenye halmashauri zao.

"Ukiona katika eneo lako biashara zinafungwa na wewe upo ni lazima ujitathmini kama unatosha, nadhani hicho ndiyo kipimo cha utendaji kazi wako, pia hapo nisisitize ni lazima mtoe elimu kwa wafanyabiashara badala ya kufikiria kuwafungia," alisema Mgumba.

Ofisa Uhusiano wa BRELA, Rhoida Andusamile, alisema mafunzo hayo yaliyowakutanisha maofisa biashara kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yamelenga kuongeza ufanisi katika masuala ya usimamizi wa biashara.

Alisema pia kupitia mafunzo hayo maofisa biashara na BRELA wamekumbushwa mipaka yao ya kazi ili kutoingiliana katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.



# SMZ: Mazingira uwekezaji yameimarishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema mazingira ya uwekezaji yameimarishwa katika kipindi cha awamu ya nane, ikiwamo fursa zinazopatikana nchini.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wametakiwa kuzitumia ili kuyafikia malengo ya uwekezaji na kukuza uchumi na maendeleo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi, Uchumi na Uwekezaji), Mudrik Ramadhan Soraga, katika kikao cha pamoja na majadiliano na watendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) kwa ajili ya kuweka mwongozo wa fursa za uwekezaji.

Soraga alisema katika kipindi cha mwaka mmoja mazingira ya uwekezaji yameimarishwa ikiwamo kuondoa urasimu kwa wawekezaji na kuifanya Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA) kuwa kituo kimoja cha uwekezaji nchini.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja ZIPA imefanikiwa kuondoa vikwazo vyote na kuifanya kuwa kituo kimoja cha uwekezaji na kumaliza mambo yote yanayowahusu wawekezaji.

Alisema wakati umefika sasa kuwapo mwongozo ambao utasaidia zaidi kujenga mazingira ya uwekezaji na kutangaza fursa zilioko nchini.

"Kikao chetu cha watendaji wa UNDP lengo lake ni kuweka mwongozo unaofahamika wenye uwazi ambao utasaidia kuweka mikakati ya uwekezaji," alisema.

Naye Mwakilishi wa (UNDP), Rukia Wadood, alisema sekta ya uwekezaji inatakiwa kuwekewa misingi mizuri ambayo itatumiwa na watu wote wenye nia ya kuwekeza.

Alisema baadhi ya nchi zimeshindwa kupata mafanikio katika sekta ya uwekezaji kwa sababu hakuna miongozo inayofahamika ya kuwekeza ambayo itatumiwa na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza.

Alipongeza hatua za awali zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ikiwamo kuifanya ZIPA kuwa kituo kimoja cha uwekezaji nchini.

"Nimefurahishwa na hatua za awali za mwaka mmoja uongozi wa awamu ya nane katika kuweka mikakati mizuri ya sekta ya uwekezaji...tunafurahi kuona ZIPA kuwa kituo kimoja cha uwekezaji nchini na hivyo kurahisisha shughuli za uwekezaji," alisema.

Alieleza kuwa UNDP ipo tayari kusaidia na kuweka mwongozo unaofahamika kimataifa katika kukuza na kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharifu Ali Sharifu, alisema wamejipanga vizuri kukifanya kituo cha uwekezaji Zanzibar kinakuwa bora Afrika chenye kuwavutia wawekezaji na kutekeleza miradi yao kwa haraka.

Alisema hivi sasa mwekezaji anaweza kumaliza mambo yake yote ya msingi katika kuwekeza miradi anayoitaka katika kipindi cha siku 3 tu....kila kitu kinapatikana ZIPA ikiwamo vibali vya ardhi," amesema.

## Matawi ya vyuo vikuu Zanzibar kufungua fursa

**Na Rahma Suleiman,**
ZAANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa, amesema ufunguzi wa matawi ya vyuo vikuu mbalimbali Zanzibar kutafungua fursa za upatikanaji wa taaluma bora nchini.

Alitoa kauli hiyo alipofanya mazungumzo na ujumbe kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na kwamba.

kupatikana kwa taaluma ya biashara kutawasaidia vijana kupunguza changamoto ya gharama za masafa.

Aidha, alisema chuo hicho kitakapoanzishwa Zanzibar kiwe na ubora sawa na huduma zake ziwe sawa na zinazotolewa Tanzania Bara.

Naye Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein, alikitaka chuo hicho kuanzisha huduma zake angalau kwa kuanzia kuwa na majengo ya kukodi, huku wakiendelea na ujenzi wa majengo yao.

Alisema wizara ipo pamoja na wadau wote wa elimu ili kuona elimu inapatikana kwa kiwango kikubwa zaidi.

Mkuu wa CBE, Prof. Emannuel Mjema, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuonyesha ushirikiano, hivyo aliahidi kuharakisha ujenzi wa chuo ili huduma zao kupatikana Zanzibar.

Akizungumzia suala la ajira, alisema ni fursa zitakazopatikana kwa wazawa na wageni katika chuo hicho kitakapoanza kutoa huduma zake.

Pia waliiomba Wizara ya Elimu kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Ofisi za Wilaya na Mkoa na wananchi wa Chwaka ili kuwapatia eneo lingine kwa sababu eneo walilonalo ni dogo.




Ofisa wa mauzo na usambazaji wa Zantel, Mwajuma Michael Mwanga, akiwasilisha mada kwa mawakala wa huduma ya EzyPesa Pemba, katika mkutano wa mwaka wa watoa huduma hiyo, uliofanyika mwishoni mwa wiki ukumbi wa Samai Gombani Chakechake Pemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Jengo la Mahakama Kuu kuwa makumbusho

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban, amesema jengo la Mahakama Kuu ya Vuga ambalo limejengwa zaidi ya miaka 200 sasa litageuzwa kuwa makumbusho ya kale.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia kukuza sekta ya utalii nchini.

Jaji huyo aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na watendaji wa Makumbusho ya Kale pamoja na Mji Mkongwe wa Zanzibar unaohusisha urithi wa kale.

Alisema Mahakama Kuu ya Zanzibar imeanza kutumia jengo jipya la kisasa lilioko Tunguu Wilaya ya Kati lenye mahitaji ya kutosha kwa watendaji pamoja na kuendesha kesi.

Alifahamisha uongozi wa mahakama kuu umewasilisha maombi Serikali Kuu na kukubaliwa kuhusu kulitumia jengo lilioko Vuga kwa matumizi ya makumbusho ya kale.

Alisema jengo hilo litatumiwa kwa ajili ya kuweka hati muhimu zinazohusiana na mahakama tangu kipindi cha tawala mbalimbali za kikoloni, hatua ambayo itawawezesha wataalamu na watu mbalimbali kufanya utafiti wa masomo yao kuhusu sheria.

"Uongozi wa Mahakama Kuu tumeanza mazungumzo na taasisi za makumbusho ya kale pamoja na uongozi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar kuhusu nia ya kuligeuza matumizi jengo la Mahakama Kuu ya Vuga na kuwa makumbusho ya utalii," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Makumbusho ya Kale, Mariamu Mansab, alisema wapo tayari kutekeleza agizo la serikali la kuligeuza jengo lililokuwa Mahakama Kuu ya Vuga kuwa jengo la makumbusho ya kale katika sheria.

Alisema jengo hilo linazo sifa zote kuwa jengo la makumbusho ya kale katika masuala ya mahakama, na kwamba ni kivutio tosha kwa watalii watakaokuja nchini na kutembelea urithi wa mambo ya kale.

Ofisa mwandamizi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe wa Zanzibar, Ali Haji, alisema jengo la Mahakama ya Vuga linakidhi vigezo na sifa za kuwa makumbusho ya kale kwa ajili ya kuwavutia watalii.

Alieleza kuwa jengo hilo litahitaji marekebisho ya mambo madogo madogo kabla ya kugeuzwa kuwa makumbusho ya kale.

Mkurugenzi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdalla Juma, alisema ni wazo zuri litakalosaidia Zanzibar kuwa na vivutio vingi vya utalii katika eneo la Mji Mkongwe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**[TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA]**

**MIRATHI NA 43 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU GODWIN THOMAS MUWOWO**
**ENEAH JORAM MUWOWO.......................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**[kanuni ya 75]**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 mwezi wa Aprili 2022.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 14 Mwezi wa Machi, 2022.

Dar es Salaam, HIGH COURT TANZANIA

NAIBU MSAJILI

---

ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULOPEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA CHAMWINO DODOMA TUTAFANYA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMAMOSI **TAREHE 26/03/2022** KUANZIA SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA MOJA ILIYOPO MTAA WA AZIMIO CHAMWINO IKULU MALI YA FANUEL SUDAY, PIA KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA MJINI TUTAUZA NYUMBA MOJA **PLOT 126 BLOCK 'C'** ILIYOPO NKUHUNGU EAST MALI YA VIOLET FELIX MUTTASSA.

**KWA MAWASILIANO TUPIGIE. NO. 0713913150**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HAPPINES GEFI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SUNLG yenye namba za usajili **MC 241 CCV** rangi nyekundu namba za Injini **156FMI-2xJ5129348**

Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Happines Gef kwa simu namba **0754375363.**

Rb namba **KHM/RB/2022** Control namba **9910831694713**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 72 YA MWAKA 2022**
**BAINA YA**
**REV.SIMON CHIWANGA ...............MKAZA HUKUMU**
**DHIDI YA**
**ELISHA KITUTU NA WENZAKE WANNE (4).......WAKAZIWA HUKUMU**

**KWA:**
**ELISHA KITUTU MKAZIWA HUKUMU NA.1**
**ROBERT LESILWA MKAZIWA HUKUMU NA.2**
**VICTAR MGANULE MKAZIWA HUKUMU NA.3**
**JUMA T.LUHUNGA MKAZIWA HUKUMU NA.4**
**MALUGU LUHUNGA MKAZIWA HUKUMU NA.5**

**POPOTE MLIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 22.03.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya mwezi Februari,2022.**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

YASIN KARAMA ABEID ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA ISUZU FORWARD YENYE NAMBA ZA USAJILI T 628 AKZ. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: KAH /TR /RB/ 174 /2022

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AZAN SAID SALUM**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 347 DCZ** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH /TR /RB/ 175/2022**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SADAT ADAM MOHAMED**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA RAV4 YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 256 DCV** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI : **KAH /TR /RB/ 161/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 109 YA 2021**
**NZIACHARO PAULO NZIACHARO NA VERONIKA MATHALIS BANZI.....................WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ATHUMANI RAMADHANI NA FABIANI JOHN...............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**RAMADHANI RAMADHANI NA FABIANI JOHN** Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 13/4/2022 mbele ya Mwenyekiti M.Khasimu ninyi wenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.

**Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 14/3/2022.**

M. KHASIMU
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

# NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Mchechu arejea rasmi, aahidi makubwa NHC

Na Christina Mwakangale

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, ameahidi kwamba tayari kuondoa vikwazo mbalimbali vitakavyojitokeza ikiwamo kukamilika kwa wakati, akisema kazi itaendelea kwa ufanisi mkubwa na kuja na ujenzi wa mpya wa makazi bora.

Amesema majiji yanahitaji kukuzwa kibiashara yenye majengo ya nyumba mpya kwa kushirikiana na wawekezaji akisisitiza mahitaji ya nyumba kuwa makubwa.

Mchechu aliyasema hayo jana kwenye taarifa yake kwa vyombo vya habari, akizungumza na wafanyakazi wa NHC Mkoa wa Dar es Salaam baada ya kuripoti ofisini tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kushika wadhifa huo.

"Tupendezeshe majiji yetu, tukuze biashara ya nyumba kwa kujenga nyumba mpya kwa ushirikiano na wawekezaji kwani mahitaji ya nyumba bado ni makubwa sana hivyo ni vyema kuwa na tafakari ya kina ili kuweza kuyafikia," alisema Mchechu.

"Ninataka yale yote tuliyoyafanya kwa miaka minane kipindi kile nikiwa NHC, yafanyike mengine makubwa kama yale kwa kipindi kifupi cha miaka minne tu, kwa maana hiyo ninasema tunahitaji kufanya kazi kwa kasi kubwa na nguvu zaidi ili kukidhi matarajio ya Watanzania," alisema Mchechu,

"Pamoja na kukamilisha miradi ya Kawe 711 na Morocco Square, wafanyakazi muwe wabunifu ili kuifikisha nchi mahala pazuri kwenye sekta ya nyumba ambayo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi.

Mchechu alibainishwa kwamba, NHC katika kipindi chake inatarajia kujenga nyumba na kuboresha makazi nchini ili kusukuma mbele malengo ya serikali, akisema miradi itamaliziwa na kuanzishwa mingine.

Aliwataka wafanyakazi kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kwamba wale wanaohisi kutoendana na kasi yake ni bora waombe uhamisho na kwamba utendaji anaoutaka ni kwa ajili ya mustakabali wa shirika na taifa.

# Mikakati 3 kukabili uhaba wa ajira

Na Christina Mwakangale

SERIKALI imesema katika kukabiliana na uhaba wa ajira nchini hususan kwa vijana, mikakati mitatu imepewa kipaumbele kuanzia sasa, ikiwamo kuanza mashauriano ya kikanda na kimataifa, kushirikiana na sekta binafsi na kulegeza masharti ya mkopo ya kibenki.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, ndiye aliyebainisha mikakati hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam, kuhusu mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, changamoto, mafanikio na matarajio ya serikali.

Alisema tatizo la ajira limekuwa la duniani kote, akisema sababu za utafiti zinabainisha kwamba, kukua kwa teknolojia na matumizi yake kwenye sekta mbalimbali yamesababisha shughuli nyingi kufanyika kisasa badala ya kutegemea nguvu kazi.

"Nguvu kazi ambayo ni vijana Tanzania Bara ni milioni 14.2 kati yao ambao ni milioni 12.5 sawa na asilimia 87.8 wana ajira. Sekta isiyorasmi inatakiwa kuwezeshwa sababu imeajiri wengi hasa vijana. Duniani asilimia 75 ya vijana wamejiajiri sekta hii na kati ya hao asilimia 96 wanatoka barani Afrika na Asia," alisema Katambi.

Katambi alisema kutokana na hilo, serikali imeamua kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana wanaohitimu elimu ya juu kupitia mpango wa mikopo ya asilimia 10 kwa kila halmashauri, na kwamba mikopo iliyokwishatolewa ni Sh. bilioni 145.8.

"Vijana kwa asilimia 30 watanufaika na fursa za zabuni. Imebainika vijana waliojiajiri sekta isiyorasmi ni asilimia 40.8 na kati ya hao kwa asilimia 16.7 wamejiajiri katika biashara ambazo aidha za kurithi katika familia zao au nyinginezo," alisema Katambi.

Pia alisema serikali inatambua ukuaji wa matumizi ya mitandao ya kijamii, akisema imeongeza ajira kwa vijana hasa katika shughuli za uandishi ingawa changamoto ni matumizi holela yasiyofuata sheria na taaluma.

"Ni uwazi kwamba mitandao ya kijamii imeajiri vijana na hauwezi kuepuka, lakini sheria ziwe thabiti. Kuna matumizi makubwa kwenye michezo ya kubahatisha, wapo wanaofanya biashara na kuuza bidhaa zao kwa kujitambulisha tu mtandaoni...hii ni fursa, na itakaposajiliwa anwani ya makazi biashara, hii taongezewa thamani na mtu kupatikana alipo," alibainisha naibu waziri huyo."




Mkurugenzi Mtendaji wa Chemba ya Biashara ya Zanzibar, Hamad Hamad (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Peak Performance International Tanzania, (PPIT), Philemoni Kisamo, wakisaini makubaliano ya kushirikiana kuendesha mafunzo ya aina mbalimbali ya kuendesha na kuleta mafanikio kwa wafanyakazi na wanachama wa Chemba ya Biashara (ZNCC). Wapili kushoto ni Mwenyekiti wa ZNCC, Ali Amour. Hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PSSSF yaanika mafanikio mwaka mmoja wa Samia

Na Maulid Mmbaga

MKURUGENZI wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Hosea Kashimba, amesema katika kipindi cha mwaka mmoja wamepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kuwaandikisha wanachama wapya 21,461 ambao ni waajiriwa wapya katika utumishi wa umma.

Akizungumza juzi katika mdahalo uliolenga kubainisha mafanikio ya mwaka mmoja wa utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan uliofanyika Azam Tv, alisema katika kipindi hicho pia wameweza kukusanya michango takribani Sh. trilioni 1.36.

Alibainisha kuwa miaka 21 iliyopita kulikuwa na michango mingi ya serikali inayokaribia Sh. trilioni 4.6 ambayo haikuingizwa kwenye mfuko kwa sababu maalum zilizokuwapo wakati huo ambapo hadi sasa Rais amelipa Sh. trilioni 2.18, huku akieleza kuwa uwezo wa mfuko kulipa umeongezeka.

"Mama pia katika kipindi hicho ameweza kulipa madeni mengine ya miradi, mifuko iliyopita ilifanya miradi kwa serikali kwa mfano ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na mingine, deni lililohakikiwa lilikuwa ni Sh. bilioni 731 awamu iliyopita ililipa Sh. bilioni 300, Mama ameingia amelipa Sh. bilioni 200," alisema Kashimba.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho pia wameweza kulipa mafao Sh. trilioni 1.84 kwa wanachama zaidi ya 57,000 na kati ya hao wamelipa wastaafu 152,000 Sh. bilioni 60 kama pensheni ya kila mwezi.

Aidha, alibadilisha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wameendelea kuwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo hati fungani za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na uwekezaji katika majengo ambapo katika ujenzi wa nyumba za kuishi wamefika asilimia 98 na za ofisi 75.

Vilevile alisema wameweza kukusanya Sh. bilioni 500 kama fedha inayotokana na uwekezaji, pia alieleza kuwa wamepiga hatua katika utoaji huduma kwa njia ya TEHAMA akibainisha kuwa lengo lao ni kufikia asilimia 100 katika mfumo huo ambapo kwa sasa wamefikia asilimia 90 za kufanya kazi bila kutumia karatasi.

# MORRISON AOMBA RADHI KIPIGO SIMBA, AFUNGUKA PIA KUFUZU

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuchapwa mabao 3-0 juzi usiku dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast katika mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa L'Amitie nchini Benin, winga wa Simba, Mghana Bernard Morrison, amewaomba radhi wanachama, wapenzi na mashabiki wa klabu hiyo huku akiahidi kuwa watafanya kila liwezekano ili kushinda mechi ya mwisho dhidi ya US Gendamarie ya Niger.

Matokeo hayo yanaifanya Simba sasa kushika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba, sawa na RS Berkane ambayo ilitoka sare ya mabao 2-2 ugenini dhidi ya US Gendamarie, lakini wawakilishi hao wa Tanzania wako nyuma kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

**Kinara wa kundi hilo ni Asec Mimosas ikiwa na pointi tisa, huku US Gendamarie inayotarajia kucheza dhidi ya Simba Aprili 3,mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwenye mechi ya mwisho ya Kundi D, ikiburuza mkia kwa alama zake tano.**

Akizungumza baada ya mchezo huo wa juzi, Morrison ambaye alitokea benchini, lakini mabadiliko yake sambamba na Taddeo Lwanga, Chris Mugalu na Peter Banda, hayakuweza kubadili matokeo siku hiyo, alisema hawakucheza vizuri na kila mmoja anaelewa wamefungwa lakini hawajatolewa.

"Tunawaomba radhi wanachama, wapenzi na mashabiki wa Simba, hatukucheza vizuri, kila mmoja anajua tumefungwa, lakini hatujatolewa. Tuna mechi dhidi ya US Gendamarie, tunaamini na tunajiamini kwamba kwenye mchezo wetu huo wa mwisho utakuwa mchezo wetu wa kufuzu, hivyo kila mmoja lazima awe imara," alisema mchezaji huyo machachari.

Kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahemed Ally, alisema kuwa wamekubali kupoteza mechi hiyo kihalali kabisa, lakini siku zote kujikwaa si kuanguka na kwa bahati nzuri, Simba inaweza kufuzu kwenda hatua ya robo fainali bila kutegemea matokeo ya timu yoyote, kama itashinda mechi yao ya mwisho.

"Hili limekwisha, hakuna muda tena wa kulijadili, matarajio yetu sasa ni Aprili 3 dhidi ya US Gendamarie, huyo ndiye mwenye tiketi yetu ya robo fainali.

Tumeanguka, tunanyanyuka, tunasonga mbele, bado tupo kwenye malengo yetu ya msimu, timu bora imepoteza mchezo, Wanasimba msihofu wala msihuzunike, ni matokeo ya mpira kwenye mashindano makubwa, tunaangalia mechi yetu ya Aprili 3 kwa Mpaka, dunia inajua nini kitatokea," alisema Meneja huyo.

# Botswana nayo yaja kuivaa Taifa Stars

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars tayari imeingia kambini kujiandaa na mechi tatu za kirafiki zilizoko kwenye Kalenda ya Fifa dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, Botswana na Sudan itakayopigwa Machi 23, 26 na 29, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema michezo hiyo iliyoko kwenye Kalenda ya Fifa wataitumia kwa mambo matatu, ambapo moja ni kuadhimisha mwaka mmoja madarakani wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

"Pia mechi hizo zitampa mwanga Kocha Kim Poulsen kuandaa kikosi chake na lingine ni sehemu ya maandalizi ya kujiandaa na kufuzu michuano ya AFCON."

"Kuhusu wachezaji si wote walioingia kambini, baadhi bado wakiwamo wachezaji wa Simba ambao wanarejea leo (jana) na baada ya hapo wataungana na wenzao kambini kwa ajili ya michezo hiyo," alisema Ndimbo.

Alisema Machi 26, mwaka huu kutakuwa na michezo miwili saa 10:00 jioni watacheza Sudan dhidi ya Afrika ya Kati na saa 1:00 usiku Tanzania itavaana na Botswana.

Ndimbo alisema tayari timu ya Taifa ya Jamhuri ya Afrika ya Kati imeshawasili nchini huku Botswana na Sudan zikitarajiwa kutua Alhamisi wiki hii kwamba viingilio katika mechi hiyo vitakuwa VIP B na C ni Sh. 5,000 na mzunguko ni Sh. 3000 huku VIP A ikiwa maalum kwa watu maalum.

**TUZO...**



Mtanzania Enekia Kasonga 'Lunyamila' (kulia), ameshinda Tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya Wanawake ya Morocco msimu wa 2021/2022. Pichani ni Enekia na mchezaji mwenzake wa Tanzania, Diana Msewa ambao wote wanaichezea Klabu ya AUSF Assa ZAG ya Morocco. **PICHA: MTANDAO**

# Klabu Ligi Z'bar kujadili mwezi wa Ramadhani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kukutana na Klabu 16 za Ligi Kuu Zanzibar ili kujadiliana kwa pamoja kuhusu michezo yao ya ligi ambayo itaingiliana na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Ligi Kuu Zanzibar inaelekea ukingoni mwa msimu wakati huu ambao tayari kila timu ikiwa imecheza michezo 24 na kubakisha sita kabla ya msimu wa 2021/22 kufikia kileleni ambapo itashuhudiwa bingwa akitia kibindoni shilingi milioni 50 kutoka kwa wadhamini wa ligi hiyo, Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa bodi hiyo, Haji Issa Kidali, alisema wanatarajia kukutana na klabu hizo kesho, Jumatano na ajenda kubwa ikiwa ni kujadili michezo ya ligi ambayo itaingiliana na mwezi wa Ramadhani kutegemea mwandamo wa mwezi, iwapo itachezwa au itasimama kupisha mwezi huo kwa kutekeleza ibada ya funga.

Alisema iwapo klabu zitakubali kucheza Mwezi wa Ramadhani, basi watafanya hivyo kama zinavyotaka, lakini itakuwa vigumu kuchezwa katika uwanja wa Gombani kutokana na uwanja huo kutokuwa na taa.

# Serikali kusaidia soka la wanawake Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Fatma Hamad Rajab, amesema wataendelea kusaidia Soka la Wanawake visiwani hapa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika kukuza sekta ya michezo kwa jinsia zote.

Fatma aliyasema alipoalikwa kuwa mgeni rasmi katika mwendelezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar kwenye mchezo uliozikutanisha timu ya Mkoani Queens na Wete Sister zote za Kisiwani Pemba, mchezo huo ukichezwa Uwanja wa Mau Kisiwani Unguja.

Katika mchezo huo ambao Mkoani Queens waliibuka na ushindi wa mabao 3-2, Fatma alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Wizara ya Michezo itakuwa mstari wa mbele katika kunyanyua soka la wanawake na kulifanya kuwa na ligi yenye ushindani na hata kupata timu bora ya Taifa.

"Nimefurahi kuona tuna timu za wanawake hapa kwetu na pia tuna Ligi ya Wanawake, ninamatumaini makubwa kupitia timu hizi na ligi hii tutapata wachezaji wazuri ambao watаunda timu ya Taifa ya Wanawake Zanzibar Queens, na timu yetu itakuwa nzuri," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CITY HAWAAMINI KWA HAALAND**
KLABU ya Manchester City haiamini kwamba ina nafasi kubwa ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland na Real Madrid wanaweza kujaribu kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kubaki Borussia Dortmund kwa msimu mmoja zaidi kabla ya kujaribu kumsajili. (***Mundo Deportivo***)

**ANCELOTTI AMTAKA BARELLA**
KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anataka kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan mwenye umri wa miaka 25, Nicolo Barella na kuwasili kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia kunaweza kuweka shaka juu ya mustakabali wa Toni Kroos mwenye umri wa miaka 32, katika klabu hiyo ya Bernabeu. (***El Nacional***)

**TCHOUAMENI AWINDWA LIVER**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni anazivutia Chelsea, Liverpool, Paris St-Germain na Real Madrid, lakini Monaco hawatakubali chini ya euro milioni 50 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. (***Foot Mercato***)

**VILLA WAMTAKA PHILLIPS**
KLABU ya Aston Villa wanaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, na wako tayari kulipa pauni milioni 60 kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (***Times***)

**DYBALA KUONDOKA JUVE**
KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amesema hajui kama mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala atakuwa katika klabu hiyo msimu ujao, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ukimalizika msimu wa majira ya joto. (***DAZN, via Football Italia***)

**HAALAND TENA MADRID**
KIUNGO wa zamani wa Real Madrid, Guti amesema klabu hiyo haitaweza kumsajili Erling Haaland iwapo itashindwa kumnasa msimu huu wa majira ya joto. (***El Chiringuito, via Goal***)

**MARCAL KUSEPA WOLVES**
MLINZI wa kushoto wa Brazil, Marcal mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kuondoka Wolves mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto na kusaini mkataba wa kujiunga na Botafogo ya nchini kwao. (***Globo Esporte***)

**KOEMAN NA UHOLANZI**
KOCHA wa zamani wa Barcelona, Ronald Koeman yuko kwenye mazungumzo kuhusu kurejea katika nafasi yake ya ukocha wa timu ya Taifa ya Uholanzi na kurithi mikoba ya kocha wa sasa wa Uholanzi, Louis van Gaal, ambaye mkataba wake unamalizika baada ya Kombe la Dunia la 2022. (***NOS***)

**MUSONDA AWANIWA ROMA**
KLABU ya AS Roma na Hellas Verona wanavutiwa na mchezaji wa Chelsea, Charly Musonda mwenye umri wa miaka 25, huku Mbelgiji huyo akitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Stamford Bridge msimu wa majira ya joto. (***Goal***)

**SIEGRIST AFUATILIWA UNITED**
KLABU ya Manchester United inamfuatilia mlinda mlango wa Uswisi, Benjamin Siegrist mwenye umri wa miaka 30, ambaye anachezea Dundee United na mkataba wake unamalizika msimu huu wa majira ya joto. (***Mirror***)

**JAMES KUJIONDOA CHELSEA**
BEKI wa kulia wa Chelsea, Reece James mwenye umri wa miaka 22, anatazamiwa kujiondoa kwenye kikosi cha England na beki wa Crystal Palace, Tyrick Mitchell (22), ataitwa kuchukua nafasi yake. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI, BUSQUETS WAANZA KUTAJA UBINGWA BARCA

**●●● Ni vigumu sana, bado tuna nafasi ndogo, lakini katika soka lolote linaweza kutokea...**

**MADRID,** HISPANIA

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi na nahodha Sergio Busquets wote hawajapuuza uwezekano wa kutwaa ubingwa baada ya ushindi wao wa mabao 4-0 dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa Clasico, Jumapili.

'Blaugrana' hao waliwaelemea Real Madrid wanaoongoza ligi kwa mabao mawili ya Pierre-Emerick Aubameyang pamoja na mawili mengine ya Ronald Araujo na Ferran Torres kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Ushindi huo unamaanisha Barcelona sasa wapo nafasi ya tatu na wamefikisha pointi 54 baada ya kucheza michezo 28, lakini bado wanaitafuta Madrid kwa pointi 12 ingawa 'Wakatalunya' hao wana mchezo mmoja mkononi.

Lakini Barcelona wamechangamshwa na mabadiliko ya kipekee katika hali yake tangu kuwasili kwa Xavi kama bosi pamoja na uhamisho wao wa Januari ambao umeongeza timu hiyo.

**Blaugrana wako kwenye mfululizo wa mechi 10 bila kufungwa kwenye LaLiga huku wakiwa wameshinda mechi tano zilizopita za ligi.**

Barcelona ina rekodi ya kushinda mara nane na sare tatu katika mechi 11 za michuano yote tangu kufungwa kwa dirisha la uhamisho la Januari, jambo linalowapa kasi.

"Sijui kama tunaweza kushinda taji, hatuwezi kukataa chochote," Xavi aliwaambia waandishi wa habari baada ya Clasico.

"Labda tumechelewa kidogo, lakini huu ni ushindi mkubwa kwetu.

"Tulikuwa bora zaidi kuliko Real Madrid. Tulicheza karibu kama timu ya nyumbani uwanjani. Ni siku ya kufurahia, si tu kama kocha wa Barca lakini pia shabiki.

"Tungefunga mabao matano au sita kwa urahisi. Tulibadilisha mwelekeo wetu mbaya wa kupoteza Clasico chache zilizopita."

Busquets alisisitiza maoni ya Xavi kwamba Barca walikuwa na matumaini ya ubingwa, ingawa ni madogo.

"Ikiwa bado tuna nafasi ndogo ya kulikimbilia taji, tutapambana hadi mwisho," alisema kiungo huyo mwenye umri wa miaka 33.

"Ni vigumu sana lakini katika soka lolote linaweza kutokea. Sisi ni Barca."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PORT VALE
VERSUS
EXETER
1 | 2.23
X | 3.19
2 | 3.14

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALLEGRI: SIJUI KAMA DYABALA ATABAKI

**TURIN,** Italia

KOCHA Massimiliano Allegri amesema kuwa hana uhakika kama nyota wa Juventus, Paul Dybala, atabakia klabuni hapo zaidi ya msimu wa majira haya ya joto, licha ya kucheka na nyavu kwenye ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Salernitana.

Nyota huyo amefunga mabao nane msimu huu akiwa na Juventus, sawa na Alvaro Morata, na zaidi ya wachezaji wengine kikosini hapo.

Hata hivyo, hii bado halijamweka mbali na kuhusishwa na uhamisho klabuni hapo.

Akizungumzia hali hiyo, bosi wa Juventus, Allegri amesema kuwa hafahamu kama nyota huyo ataendelea kuwapo baada ya msimu huu wa majira ya joto.

"Sifahamu kama ataendelea kuwa mchezaji wa Juventus au la! Ndiyo maana tuna klabu na mimi nipo katika mstari huo. Si Paulo (Dybala) pekee mkataba wake unakaribia kuisha, pia kuna Juan Cuadrado, Federico Bernardeschi na De Sciglio," alisema Allegri.

"Kwa upande wangu, na kwa upande wa timu, kuna suala la nia ya kufanya vizuri pekee. Ninafanya tathmini ya wachezaji, lakini kuna masuala mengi ikiwa ni pamoja na mikataba."

Dybala amekuwa akihusishwa na Liverpool.





## Ronaldo kubaki Man United

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, anakusudia kubaki kwenye klabu hiyo hata kama haitafuzu kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa kutoka nchini Ureno amerudi kwenye dimba la Old Trafford, baada ya miaka 16 aliyotumia nje ya Man United na kwa mara ya kwanza atamaliza msimu pasipo taji lolote ndani ya miaka 16.

Ingawa Man United inasuasua, lakini Ronaldo amepanga kubaki kwenye kikosi cha Mashetani Wekundu hao kwa msimu ujao, hata kama ikishindwa kufuzu kushiriki mashindano ya Ulaya.

Man iliondolewa kwenye michuano hiyo na Atletico Madrid kwa ushindi wa bao 1-0 katika mchezo wa pili uliochezwa kwenye dimba la Old Trafford, ikiwa ni baada ya ule wa awali ugenini kumalizika kwa sare ya 1-1 kwenye hatua ya 16-bora.

Ushiriki wa Man United kwa msimu ujao kwenye mashindano hayo uko shakani, baada ya kuwa nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu England nyuma ya Arsenal, ambayo inashika nafasi ya nne huku ikiwa na mchezo mmoja mikononi.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# BONDIA NGWANDO AFANYA KWELI 'FAINALI ZA CHAMPION WA KITAA'

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa Tanzania, Ally Ngwando ameibuka bingwa wa mkanda wa PST katika uzani wa Kg. 51 kwa kumchapa kwa pointi James Kibazangwe kwenye pambano kali la raundi nane kuwaniwa ubingwa huo.

**Katika pambano hilo la 'Fainali za Champion wa Kitaa', lililofanyika juzi katika Uwanja wa Ndani wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam, Ngwando alishinda kwa pointi kwa majaji wote watatu baada ya kumpa alama 76, 77 na 78.**

Mbali na pambano hilo la Ubingwa wa PST, kulikuwa na mapambano mengine ikiwamo bondia Adam Mbeya ambaye alimchapa Hassan Ndonga kwa KO katika raundi ya nne, akianguka mara tatu na kuhesabiwa.

Katika pambano lingine siku hiyo, bondia Hassan Kibu alilazimika kukimbizwa Hospitali ya Rufani Temeke baada ya kuangukia kichwa kutokana na ngumi kali aliyopigwa na Max Mushi.

Kibu aliangukia kichwa na mgongo, hali iliyosababisha kupoteza fahamu licha ya kupewa huduma ya kwanza kabla ya kukimbizwa katika Hospitali ya Temeke na baadaye kupewa rufani ya kwenda Muhimbili.

Bondia Mussa Dragon, mambo yalikuwa magumu kwa upande wake baada ya kukubali kipigo cha TKO ya raundi ya tano kutoka kwa Selemani Galile katika pambano la raundi sita.

Dragon amezoeleka kwa kuchapa KO za mapema, lakini katika fainali za Champion wa Kitaa, alikutana na dhoruba hiyo. Pia pambano kati ya Yuko Mchawi na Mohammed Changondo lilimalizika kwa sare ya 'No Contest' (Hakuna Shindano), baada ya Changondo kumpiga ngumi Mchawi akiwa ameteleza na kudondoka chini.

Pambano lingine ambalo lilichukua taswira ya pekee ni kitendo cha bondia Saidi Mkola baada ya kumpiga Hamad Mkude na kushangilia kwa staili ya mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele.

Akizungumza na gazeti hili Mwandaaji wa pambano hilo, Selemani Semunyu, alisema lengo la Champion wa Kitaa ni kuibua vipaji vipya ambavyo vipo mtaani, lakini havionekani kwa sababu ya mabondia kukosa fursa.

"Huu ni mwanzo tu wa Pambano la Champion wa Kitaa, tulifanya kwa udogo ila mashabiki watuliheshimisha na kulifanya jambo hili kuwa kubwa, naamini mwakani mambo yatakuwa mazuri zaidi," alisema Semunyu.

Alisema pambano hilo wamechagua mabondia watatu waliofanya vizuri na kwenda kuonyesha burudani nzuri, Morogoro katika pambano la bondia Twaha Kassim 'Twaha Kiduku' dhidi ya Alex Kabangu kutoka Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC).




Ally Ngwando akizuia konde kutoka kwa James Kibazangwe katika Fainali za Champion wa Kitaa zilizofanyika Uwanja wa Ndani wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam juzi. Ngwando aliibuka Bingwa wa Mkanda wa PST. **NA MPIAGAPICHA WETU**

# Kibadeni amvulia kofia Manula

**Na Adam Fungamwango**

MMOJA wa wachezaji bora nchini miaka ya 1970 wa Klabu ya Simba na timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Abdallah Kibadeni, amemvulia kofia golikipa namba moja nchini, Aishi Manula, akisema kwa sasa yupo kwenye kiwango cha juu na amekomaa.

Kibadeni, mchezaji pekee ambaye mpaka sasa amefunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi za watani wa jadi, Simba na Yanga, mwaka 1977, kwenye ushindi wa mabao 6-0 walioupata, amesema uwezo alioonyesha Manula kwenye mechi ya juzi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, unaonyesha ameshafikia daraja la kuwa mmoja wa makipa bora kabisa barani Afrika.

"Kusema kweli Manula kwa sasa yupo kwenye kiwango cha juu sana, si Tanzania bali Afrika, na amekomaa tayari kwa sababu golikipa kila anavyodizi kukaa golini na umri unavyozidi kuongezeka ndivyo anakuwa bora zaidi, mwanzo alikuwa kijana mdogo, lakini sasa ameshakomaa, ni msaada mkubwa kwa Simba na timu ya taifa," alisema Kibadeni ambaye pia ni kocha wa zamani wa timu hiyo.

Kuhusu mechi hiyo, Kibadeni alisema kuwa Simba ilifungwa mabao 3-0 kutokana na makosa waliyoyafanya mwanzoni mwa mchezo na kuruhusu mabao mawili ya haraka.

"Pale sasa hata mimi mwenyewe nilishindwa kuangalia huo mpira, maana mabao mawili ya haraka kwa muda kama ule, nikajua kabisa leo hapa yatakuwa mengi, lakini vijana walijitahidi, hasa Manula ambaye ametuondolea aibu, tungeweza kufungwa mabao mengi," alisema.

Kipa huyo, mbali na kuokoa michomo ya hatari, aliokoa penalti mbili za Asec Mimosas, moja kila kipindi na kuiokoa Simba ambayo ilikuwa inaelekea kupata kipigo cha mabao 5-0.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 22/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4717 | Carsambaspor vs Bayrampasa | 3.00 | 2.95 | 2.60 |
| 16:15 | 5097 | AL Ain vs AL Sahel SC | 2.71 | 2.81 | 2.66 |
| 16:20 | 4168 | Al Orubah vs AL Khlood | 2.10 | 2.95 | 3.53 |
| 16:30 | 2818 | Ohud Medina vs AL Jeel | 1.54 | 3.86 | 5.20 |
| 17:00 | 1361 | MSK Namestovo vs MFK Dubnica | 5.20 | 4.14 | 1.50 |
| 17:00 | 4025 | Sheffield United U23 vs Colchester U23 | 1.31 | 5.20 | 6.93 |
| 18:30 | 1055 | AL Nahdha vs Najran SC | 2.95 | 2.85 | 2.65 |
| 20:00 | 2969 | FC KoÅiice vs MFK Skalica | 2.08 | 3.38 | 3.09 |
| 21:00 | 1628 | Deportivo Espanol vs UAI Urquiza W | 9.64 | 6.55 | 1.19 |
| 21:00 | 3715 | SV Heimstetten vs 1860 Rosenheim | 1.51 | 4.23 | 4.99 |
| 21:00 | 5406 | SV Tasmania Berlin vs Carl Zeiss Jena | 8.44 | 5.56 | 1.25 |
| 21:00 | 5973 | Castanhal EC PA vs Aguia de Maraba PA | 1.78 | 3.17 | 4.51 |
| 22:00 | 4925 | Harrogate vs Leyton Orient | 2.40 | 3.20 | 2.85 |
| 22:05 | 1528 | Flandria vs Estudiantes BA | 2.75 | 2.84 | 2.60 |
| 22:05 | 5937 | Dunfermline vs Partick Thisle | 3.02 | 3.17 | 2.28 |
| 22:45 | 1166 | Stirling vs Albion Rovers | 1.81 | 3.51 | 3.80 |
| 22:45 | 1274 | Concord Rangers vs St.Albans | 2.66 | 3.38 | 2.34 |
| 22:45 | 1314 | Newtown AFC vs Penybont | 2.00 | 3.46 | 3.22 |
| 22:45 | 1408 | Witton Albion vs Stafford Rangers | 3.37 | 3.41 | 1.96 |
| 22:45 | 1499 | Maidenhead U vs Southend | 2.84 | 3.23 | 2.36 |
| 22:45 | 1712 | Woking vs Weymouth | 1.63 | 3.81 | 4.78 |
| 22:45 | 1967 | East Thurrock vs Cheshunt | 4.43 | 4.23 | 1.57 |
| 22:45 | 1996 | Enfield Town vs Leatherhead | 1.23 | 5.19 | 10.57 |
| 22:45 | 2222 | Brackley Town vs Alfreton | 1.53 | 3.94 | 5.19 |
| 22:45 | 2307 | Spennymoor Town vs AFC Fylde | 3.52 | 3.47 | 1.90 |
| 22:45 | 2327 | Eastleigh vs Dagenham and Redbridge | 3.14 | 3.38 | 2.13 |
| 22:45 | 2452 | Blyth Spartans vs Bradford PA | 2.20 | 3.42 | 2.84 |
| 22:45 | 2466 | Plymouth vs Cheltenham | 1.76 | 3.64 | 4.23 |
| 22:45 | 2642 | Stalybridge vs Mickleover Sports | 2.15 | 3.55 | 3.20 |
| 22:45 | 2702 | Grimsby vs Solihull Moors | 2.13 | 3.27 | 3.22 |
| 22:45 | 2825 | Darlington vs Southport | 2.12 | 3.42 | 2.98 |
| 22:45 | 2893 | Wrexham vs Halifax | 1.68 | 3.58 | 4.80 |
| 22:45 | 2984 | Altrincham vs Chesterfield | 3.47 | 3.57 | 1.94 |
| 22:45 | 3192 | Gateshead vs Curzon | 1.42 | 4.51 | 5.76 |
| 22:45 | 3476 | Notts County vs Boreham Wood | 1.88 | 3.41 | 3.85 |
| 22:45 | 3886 | Yeovil vs Bromley | 2.52 | 3.25 | 2.62 |
| 22:45 | 4079 | Atherton Collieries vs Gainsborough | 2.17 | 3.47 | 2.85 |
| 22:45 | 4362 | Torquay vs Aldershot | 1.67 | 3.67 | 4.70 |
| 22:45 | 4365 | Bognor Regis vs Merstham | 1.76 | 3.46 | 4.13 |
| 22:45 | 4431 | Dungannon Swifts vs Cliftonville Belfast | 10.64 | 5.80 | 1.20 |
| 22:45 | 4628 | Warrenpoint vs Coleraine FC | 5.04 | 4.17 | 1.51 |
| 22:45 | 4739 | Kings Lynn vs Stockport | 9.36 | 5.46 | 1.26 |
| 22:45 | 4799 | Farnborough Town vs Dorchester Town | 1.41 | 4.90 | 6.80 |
| 22:45 | 4948 | Oldham vs Sutton United | 3.28 | 3.38 | 2.09 |
| 22:45 | 5018 | Port Vale vs Exeter | 2.23 | 3.19 | 3.14 |
| 22:45 | 5181 | Guiseley vs Telford | 2.30 | 3.27 | 2.79 |
| 22:45 | 5371 | York City vs Boston Utd | 1.97 | 3.37 | 3.37 |
| 22:45 | 5862 | Gloucester City vs Chester | 1.94 | 3.47 | 3.38 |
| 22:45 | 5998 | Rochdale vs Mansfield | 2.43 | 3.20 | 2.81 |
| 23:00 | 2242 | Tigres FC (COL) vs Chico | 4.83 | 3.28 | 1.70 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Machi 22, 2022

Nipashe



Ronaldo kubaki Man United UKURASA 22

# SIMBA SASA YAITANGAZIA 'KIAMA' GENDARMERIE

## ●●● Yasema itakuwa ni fainali ya CAF, kutua leo huku Pablo akitoa sababu tatu kipigo Asec, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kukubali kichapo cha mabao 3-0 katika mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast juzi nchini Benin, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amekubali kubeba lawama zote za kupoteza mchezo huo, huku akitoa sababu za kipigo hicho na kuahidi kufanya kweli Aprili 3, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba ambayo kwa sasa inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba sawa na RS Berkane ya Morocco, itahitimisha hatua hiyo ya makundi nyumbani dhidi ya US Gendarmerie ya Niger katika mechi itakayopigwa majira ya saa 1:00 usiku, wakati huo huo Wamorocco hao nao wakiwa kwao kumalizana na Asec Mimosas inayoongoza Kundi D ikiwa na alama tisa.**

Ili Simba kufuzu hatua ya robo fainali inapaswa kushinda dhidi ya US Gendarmerie, matokeo ambayo yataifanya kufikisha pointi 10 zinazoweza kufikiwa na RS Berkane kama ikishinda au Asec Mimosas ikitoka sare, lakini Waivory Coast hao wanaweza pia kupita na kufisha alama 12 endapo watashinda mchezo wao huo wa mwisho ugenini nchini Morocco.

Ikumbukwe kila kundi timu mbili zinazoshika nafasi ya kwanza na ya pili zinafuzu robo fainali, hivyo sare yoyote kwa Simba, itaifanya kuaga michuano hiyo, lakini RS Berkane inatakiwa nayo kushinda ili kufuzu huku sare yoyote kwa Asec Mimosas ikiwapa tiketi ya kusonga mbele.

Akizungumza na mwandishi wetu, Pablo alisema walipoteza kutokana na kutocheza vizuri katika mchezo huo dhidi ya Asec na huku wakipoteza nafasi nyingi za kufunga, jambo ambalo unapofanya hivyo ukiwa ugenini lazima uadhibiwe.

Alisema kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu kwao kutokana na kucheza vibaya na wenyeji kutawala mchezo hivyo kupata mabao mawili ya haraka, lakini cha pili walirudi vizuri ila tatizo lilikuwa kushindwa kutumia nafasi walizotengeneza.

"Hatukucheza vizuri, tofauti na matarajio yetu, kipindi cha kwanza Asec walitawala mchezo na kupata mabao mawili, lakini cha pili tulipoteza nafasi, kama kocha nakubali kubeba lawama kwa kilichotokea ila wachezaji wangu nao wanapaswa kupambana kwa sababu wanacheza timu kubwa," alisema Pablo.

Katika kuonyesha kuunga mkono kauli hiyo ya Pablo, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, ameisindikiza kwa kueleza kwamba hawapaswi kulaumiana wala kunyosheana kidole kwa matokeo hayo bali kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao wa mwisho.


Barbara alisema bado wana nafasi ya kutinga robo fainali na kutimiza malengo yao kama watajipanga vizuri na kushinda mchezo wa mwisho dhidi ya US Gendarmerie, hivyo hawapaswi kupoteza lengo kwa sasa.

"Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, bado tuna nafasi ya kutinga robo fainali kama tutashinda mchezo wetu wa mwisho, hivyo wachezaji walioitwa timu zao za taifa wataenda kujiunga nazo baada ya kuwasili leo na ambao hawako katika majukumu na timu zao za taifa watapata mapumziko mafupi kabla ya wote kurejea kambini Machi 27, kujiandaa na mechi dhidi ya US Gendarmerie," alisema.

Kwa upande wa winga wa Simba, Mghana Bernard Morrison, amewaomba radhi wanachama, wapenzi na mashabiki wa klabu hiyo huku akiahidi kuwa watafanya kila liwezekanalo ili kushinda mechi ya mwisho dhidi ya US Gendamarie ya Niger.

"Tunawaomba radhi wanachama, wapenzi na mashabiki wa Simba, hatukucheza vizuri, kila mmoja anajua tumefungwa, lakini hatujatolewa. Tuna mechi dhidi ya US Gendamarie, tunaamini na tunajiamini kwamba kwenye mchezo wetu huo wa mwisho utakuwa mchezo wetu wa kufuzu,

**TULIA DOGO...**



Winga wa Taifa Stars, Simon Msuva akimiliki mpira dhidi ya straika George Mpole, wakati wa mazoezi ya timu hiyo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, kujiandaa na mechi tatu za kimataifa za kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudan na Botswana zitakazopigwa uwanjani hapo kuanzia wiki hii. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Nabi aanza hesabu za Azam FC, Simba


**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameanza kupiga hesabu nzito za kuvuna pointi sita katika michezo miwili iliyombele yao dhidi ya Azam FC na Simba, ambayo anaichukulia kama fainali kwao kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inayoongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 48, huku ikiwa na kibarua dhidi ya Azam FC mchezo utakaopigwa Aprili 6, katika Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam na baada ya hapo itakutana na Simba Aprili 30, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kila mechi kwao ni fainali, lakini michezo hiyo miwili ni migumu zaidi hasa kulingana na ubora wa timu hizo.

Alisema licha ya kupata matokeo mazuri katika michezo yao 18, hawako katika ubora sana wakuweza kuwafanya kuwabeza wapinzani wao, hivyo wanapaswa kuwaheshimu ili kuhakikisha wanapata pointi katika mechi hizo.



"Hizi ni mechi ngumu kuna Azam FC na Simba hasa ukizingatia ni 'Derby', ndio kubwa kwa Afrika na huchukuliwa kwa umuhimu hali ambayo kila mmoja anahitaji kupata pointi kufikia malengo yake," alisema Nabi.

Alisema anaamini mechi hizo ni muhimu kuanza kujipanga mapema ili kuhakikisha wanaweka mikakati yao imara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >